SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mwinyi** aweka wazi sababu kuwatumbua watendaji wa serikali

UKURASA 17


# Nipashe

Jumatatu Septemba 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580709

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




11 bora yenye thamani kubwa EPL kwa sasa

UKURASA 12



# Rugemalira atoa ahadi kwa serikali

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MANISPAA YARIDHIA GULIO NGUO MACHINGA**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imeridhia kufanyika kwa...

UKURASA WA 18

**CHONGOLO AONYA WANAOCHAGUA VIONGOZI CCM**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo...

UKURASA WA 18

**WAZIRI ATILIA SHAKA WANASIASA WALIOPITA**

SERIKALI imesema maamuzi ya wanasiasa nchini yalichangia kuua...

## BAWACHA: Tunalaani polisi kwa kutuvuruga

UKURASA 2



Timu ya mafundi na waokoaji katika mgodi wa Nyandolwa wilayani Shinyanga, wakiingia shimoni kuokoa watu waliofukiwa na kifusi, wanne waliokolewa katika mashimo hayo ya dhahabu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MOHABU DOMINIC**

# Waziri: Siogopi vitisho

UKURASA 2

**MICHEZO** AZAM YAGEUKIA VPL, YAIPOTEZEA PYRAMIDS UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

## BAWACHA yalaani polisi kuwavuruga

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), limelaani kitendo cha Polisi kuvuruga mazoezi ya kukimbia yaliyokuwa yakifanywa na kikundi cha mazoezi cha baraza hilo.

Baraza hilo lilisema tukio hilo ambalo lilitokea juzi, Jimbo la Kibamba mkoani Dar es Salaam na kudai kwamba Polisi wote waliohusika kusambaratisha kikundi hicho walikuwa wa kiume kinyume na kanuni za kijinsia.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyosainiwa na Kaimu Mwenyekiti BAWACHA Tanzania, Sharifa Suleiman, kitendo kilichofanywa na polisi hao siyo cha kidemokrasia bali kina viashiria vya unyanyasaji wa kijinsia.

"Mazoezi haya ni jambo la kawaida ambalo wanawake wamejipangia kufanya kila wiki kwa ajili ya kuimarisha afya zao. Vitendo hivi vimekuwa vinalenga matukio yanayofanywa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) huku wengine wakiendelea na mazoezi hayo na mikutano ya ndani na hadhara bila kubughudhiwa kwa namna yoyote na jeshi hilo," alisema Sharifa.

Aidha, alisema baraza linalaani pia matumizi ya polisi wanaume kunyanyasa raia wa kike kwa kuwa ni udhalilishaji na kwamba BAWACHA haitaendelea kuvumilia vitendo hivyo linafanya mashauriano na wanasheria wake juu ya hatua za kuchukua dhidi ya polisi wanyanyasaji.

"BAWACHA itaendelea kuwa na staha, imara kulinda heshima ya akina mama wanawake wote nchini dhidi ya vitendo vyote vya udhalilishaji na kuonewa. Ni bahati mbaya kwamba katika kipindi hiki, wakati nchi inapitia kwenye changamoto hizi za unyanyasaji wa polisi dhidi ya raia, Rais Samia Suluhu Hassan amesafiri kwenda New York, Marekani kuhudhuria na kuhutubia Mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN)." Aidha, aliongeza kwamba BAWACHA inasisitiza kwa namna yoyote ile, wakati rais akipata fursa ya kujumuika na viongozi wenzake ni vyema kutambua raia wa Tanzania wana haki ya kujumuika na viongozi wenzake kwa uhuru bila kubughudhiwa.

"Sisi kama wazazi na walezi hatupo tayari kuona nchi yetu inadidimia katika lindi la ukatili, unyanyasaji na uonevu wa dola dhidi ya raia. Tutailinda nchi yetu katika wakati huu wa maambukizi ya corona tutaendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kujali afya. Hivyo, licha ya fujo za polisi dhidi ya akina kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kujali afya.

# Rugemalira atoa ahadi kwa serikali

**Na Romana Mallya**

MFANYABIASHARA James Rugemalira, aliyeachiwa huru na mahakama dhidi ya kesi ya uhujumu uchumi, amemshukuru Mungu kanisani pamoja na serikali na kuahidi kuwa yuko tayari kushirikiana kuijenga nchi.

Alitoa shukrani hiyo jana katika misa ya pili aliyoshiriki na familia yake katika kanisa analoabudu la Katoliki Makongo Juu, Parokia ya Bikira Maria Mama wa Rozari Takatifu.

Alisema amesamehe na kazi yake kubwa ni kumwomba Mungu.

Mfanyabiashara huyo ambaye alikaa ndani gerezani kwa miaka minne akisubiri upelelezi wa kesi yake iliyokuwa ikimkabili, alimshukuru Paroko wa kanisa hilo, Joseph Masenge kwa kumtembelea wakati akiwa gerezani na kumwombea.

Katika ibada hiyo ya kushukuru pia, hakuwasahau waumini wenzake kwa kumwombea wakati wote akiwa katika matatizo mpaka alipoachiwa kuwa huru.

Alhamis iliyopita, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ilimwachia huru mfanyabiashara huyo baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati ya Nole chini ya kifungu cha 91(1) ya kuonyesha hana nia ya kuendelea na mshtakiwa Rugemalira. Kesi hiyo ilipangwa siku hiyo kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi, Huruma Shaidi.

Mfanyabiashara huyo alikuwa mahabusu gerezani kwa takribani miaka minne na miezi mitatu.

Alishikiliwa kwa uchunguzi wa kesi yake tangu Juni, mwaka 2017, alipopandishwa kizimbani kusomewa mashtaka dhidi ya uhujumu uchumi. Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, alidai mahakamani hapo kwamba kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa.

"DPP hana nia ya kuendelea na kesi hii dhidi ya Rugemalira, tunaomba Mahakama imwachie," alidai Wakili Mwanga, wakati akisoma maelezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Katika kuonyesha shukrani kwa Mungu kwa kuachiwa huru, alipotoka mahakamani alikwenda moja kwa moja kwa kanisa lake alilokuwa akiabudu yeye na familia yake na baadaye nyumbani kwake.

Katika kesi hiyo Rugemalira alikuwa anakabiliwa na mashtaka 12, ikiwamo la utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.6 na Sh. 309,461,300,158.27.

Katika kesi hiyo pia mfanyabiashara mwingine Herbinder Seth, aliunganishwa katika mashtaka hayo.

Seth aliachiwa huru Juni 21, mwaka huu na kutakiwa kutotenda kosa lolote kwa kipindi cha mwaka mmoja na pia alitakiwa kuilipa fidia serikali ya Sh. bilioni 26.9 baada ya kuandika barua kwa DPP ya kukiri mashtaka.



Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya, akizungumza wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Wanahisa wa Benki ya Mwanga Hakika Microfinance Bank (MHB) uliofanyika jana, wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mhandisi Ridhuan Mringo na kushoto ni Katibu wa Benki hiyo, Nancy Kissanga. Mkutano huo ulilenga kujadili mikakati ya benki katika ukuzaji wa huduma za hapa nchini. **ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Simbachawene: Siogopi vitisho

**Na Felix Mwagara,** KIBAKWE

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema kuwa ataendelea kukemea matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na hataogopa vitisho vya mtu yeyote kwa kuwa ameapa kupambana na uhalifu wa aina mbalimbali nchini.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Kidenge, Kata ya Luhundwa, Jimboni kwake Kibakwe, wilayani Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma, Waziri Simbachawene alisema baadhi ya watu wamepotosha kauli yake, huku wakisem anaingilia uhuru wa vyombo vya habari.

Alisema wanaopotosha wana malengo yao, kwa kuwa msingi wa hoja yake ni wahalifu wa mitandaoni na siyo vinginevyo.

"Ninaposimama kama Waziri niliyeapa kwa ajili hiyo, nasema tutumie mitandao hiyo vizuri, tutumie mawasiliano ya simu vizuri, tusiwaibie watu, wanaofanya hivyo wanafanya makosa, wachukuliwe hatua za kisheria," alisema na kuongeza;

"Wanaotumia mitandao kutukana wenzao, kukashifu wenzao, kurusha picha za hovyo, wanafanya makosa maana jamii yetu imejengeka katika misingi, utaratibu na utamaduni wa kuheshimiana, eti naingilia uhuru wa vyombo vya habari, huko ndivyo wanavyojadili kwamba Simbachawene sasa naye atapoteza umaarufu kwa sababu anaingilia uhuru wa vyombo habari."

Aidha, alisema mitandao ya kijamii ni hatari kwa maendeleo ya nchi endapo itatumiwa vibaya kwa kuwa nchi haitakiwi kufika huko na ndiyo maana serikali iko macho, na kwamba ameshatoa maelekezo ya kupambana na wahalifu wanaotumia vibaya mitandao.

"Kuna rafiki yangu mmoja kanipigia simu kaniambia eti Simbachawene huko usiende sisi tunakutegemea sana, acha watu waseme, watu waseme wanawatukana wenzao?, watu waseme wanawaibia wenzao?," alifafanua na kuongeza:

Mimi nazungumzia uhalifu, sijazungumzia maendeleo ya sayansi na teknolojia, maendeleo ya mwasiliano yatabadilika, mikutano kwenye 'twiter', kwenye 'space conference' itaendelea tu, lakini itumike kwa mujibu wa taratibu zilizopo, staha na kuweka heshima ya kitanzania mbele."

Kwa mujibu wa Waziri huyo, ni kosa kutumia mitandao ya kijamii kuvunja sheria za nchi kwa kuwanyima watu wengine raha kwa kisingizio cha uhuru maoni.

"Kila mtu anahitaji kuheshimiwa, siyo unatukana, unakashifu, tena unaowakashifu ni viongozi, hata kama siyo kiongozi mtu anastahili haki yake ya kuheshimiwa," alisisitiza Waziri Simbachawene.

"Eti wanasema nitafunga 'social media' (mitamdao ya kijamii), mimi nimesema nitafunga 'social media'? Mimi sijasema nitafunga 'social media', mimi nimesema tutumie kwa kuzingatia sheria, tusitumie kwa kuvunja sheria za nchi na kukashifu na kuwanyima watu wengine raha kwa kisingizio kwamba uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kutoa maoni upo, 'social media' zipo, zitaendelea kuwapo, lakini lazima tuzitumie kwa uangalifu kwasababu zinaweza kuvunja umoja na mshikamano wa kitaifa," alibainisha Simbachawene.

Aidha, Waziri Simbachawene alirudia kauli yake ya kulitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua kali wanaotumia mitandao ya kijamii kufanya uhalifu ikiwemo kumkashifu na kumtukana Rais.

"Rais ni kiongozi wetu, amewekwa na Mungu, kumbeza kumtukana, kumkashifu, kumdhalilisha ni kosa, na unapomdhalilisha unalidhalilisha taifa, hao wanaofanya hivyo na pia hata kwa viongozi wengine wote tutawashughulikia," alisema Simbachawene.

Aidha, Waziri huyo ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, alisema kwa miezi mitano wananchi hao wamepewa zaidi ya Sh. bilioni mbili za miradi ya barabara na kati yake Sh. Milioni 500 ni za ujenzi wa barabara yenye urefu wa Kilomita 1.3 mjini humo.

Pia, zaidi ya Sh. milioni 260 wa ajili ya maendeleo ya miradi mbalimbali katika kata ya Luhundwa.

"Fedha hizo bilioni mbili za barabara tayari tumezigawa katika mchanganuo na tutakwenda kuzirekebisha barabara zetu pamoja na maeneo ambayo hatujayafungua tutayafungua," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mkutano wa UN utakavyoinufaisha Tanzania

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, ameeleza Tanzania itakavyonufaika Rais Samia Suluhu Hassan, kuhudhuria kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) kitakachoanza Septemba 21 hadi 27, mwaka huu jijini New York, Marekani.

Msigwa alisema, katika mkutano huo wa 76 wa UN kuna kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Rais Samia atahutubia Septemba 23, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, alisema manufaa ni pamoja na kujua nchi zenye uhaba wa chakula na kuwa Tanzania imezalisha zaidi itapata fursa za masoko.

"Kikao hiki kitakuwa na kaulimbiu inayohusu kujiimarisha baada ya madhara yanayosababishwa na ugonjwa wa corona (Uviko-19), kuweka mipango ya kukabiliana na athari zake, kukabiliana na mahitaji ya dunia na haki za watu na maisha mapya ya umoja wa mataifa baada ya kukumbwa na janga la ugonjwa huu," alisema Msigwa.

Alisema kutokana na athari mbalimbali za ugonjwa wa corona duniani pia mataifa mengi yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa chakula.

Msigwa alisema kutokana na Tanzania kuvuna ziada ya tani za mazao ya mahindi pamoja na mchele kupitia mkutano huo itapata fursa ya soko kuuza chakula katika nchi zenye uhaba.

"Sasa tukumbuke huu ni mkutano wa kwanza kufanyika ana kwa ana tangu ugonjwa huu uliipoikumba dunia na ni mkutano muhimu ambapo viongozi wanakwenda kubadilishana mawazo na uzoefu juu mafunzo waliyoyapata na kuweka mikakati ya pamoja ya namna ya kukabiliana nao," alisisitiza Msigwa.

Vilevile, alisema pamoja na kushiriki kikao hicho cha Baraza Kuu, Rais Samia pia atashiriki vikao vingine vya kimataifa ambavyo ni kikao cha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), kikao cha masuala ya usalama wa chakula na kikao cha masuala ya mabadiliko ya tabia nchi.

"Pia Rais Samia, atashiriki vikao vya uwili (Bilaterals), yaani kukutana na viongozi mbalimbali, huku kote anakwenda kusimamia maslahi ya nchi yetu," alisisitiza Msigwa.

Akizungumzia hali ya uwekezaji nchini, alisema ni ajenda iliyoendelea kupewa umuhimu wa kipekee na serikali ya awamu ya sita.

"Nafurahi kuwaambia kuwa juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususani sekta binafsi zimeendelea kuzaa matunda, uwekezaji unaendelea kufanyika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii licha ya dunia ikiwamo Tanzania kukabiliwa na changamoto zinazosababishwa na janga la ugonjwa wa Uviko-19," alisema.

Alisema katika mwaka 2020/21 Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kilisajili miradi mipya 235, ikilinganishwa na 219, iliyosajiliwa mwaka 2019/20.

Alisema taarifa ya uwekezaji ya dunia ya mwaka 2020, inayotolewa na Shirika la Maendeleo na Biashara la Umoja wa Mataifa (UNCTAD) imeonyesha Tanzania ilipokea uwekezaji wa Dola za Marekani bilioni moja sawa na Sh. trilioni 1.235 katika mwaka huo na kuongoza kwa kupata uwekezaji wenye thamani kubwa katika Afrika Mashariki.

"Sasa mwaka huu ambapo nchi yetu imekumbwa na wimbi la nne la Uviko-19 hali ipoje? Kati ya Machi na Agosti, 2021 TIC imesajili miradi mipya 133, ambayo inatarajiwa kuzalisha ajira 29,709 ikilinganishwa na miradi 105 iliyosajiliwa mwaka jana 2020, katika kipindi kama hicho ambayo imezalisha ajira 8,252," alisema.

# Serikali kuendelea kuwalinda wenye viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kuwalinda wenye viwanda nchini na haitavumilia kuona wawekezaji wakinyanyaswa.

Pia Waziri Mkuu amesema Rais Samia Suluhu Hassan amewaagiza wasaidizi wake wasimamie mwenendo mzima wa masoko ya mazao mbalimbali nchini likiwamo na zao la kahawa, ili kuhakikisha wakulima wananufaika na kazi wanayoifanya.

Majaliwa ameyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi baada ya kukagua kiwanda cha kuchakata kahawa cha Ngara Coffee kilichoko wilayani Ngara mkoani Kagera.

Alisema Rais Samia ameendelea kuwahamasisha wawekezaji waje nchini na wawekeze katika sekta mbalimbali ikiwamo ya viwanda ambavyo vitawawezesha wakulima kupata masoko ya uhakika ya mazao yao.

Akizungumzia kuhusu kiwanda hicho, Waziri Mkuu amewasisitiza wananchi wa Ngara watumie fursa ya uwepo wa kiwanda cha Ngara Coffee kwa kuongeza ukubwa wa mashamba ya kahawa kwa kuwa wana soko la uhakika.

Waziri Mkuu alisema uzalishaji wa kahawa kwa wilaya ya Ngara ni tani 1,000 kwa mwaka kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na uwezo wa kiwanda hicho, hivyo amewashauri wakulima waongeza uzalishali ili kukiwezesha kiwanda hicho kupata malighafi ya kutosha.

Kadhalika, Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali, Charles Mbuge, aunde timu maalumu itakayofanya mapitio ya mfumo mzima wa uuzaji wa zao la kahawa wilayani Ngara.

Ametoa agizo hilo baada ya kutoridhishwa na mwenendo wa uuzaji wa zao hilo unaosimamiwa na Chama cha Msingi cha Wakulima wa Kahawa Ngara ambacho kimekuwa kikiwakata wakulima makato mengi na kuwapunguzia tija.

"Makato mengi mnayowakata wakulima hayana msingi kwa mkulima, mfano wa makato hayo ambayo yanakatwa katika kila kilo moja ya kahawa ya mkulima ni pamoja na riba ya mkopo unaokopwa na chama hicho (36%), usafirishaji (34%), gharama za ukoboaji (shilingi 112), gharama ya usafirishaji nje (1%)."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa kiwanda cha Ngara Coffee, Abdallah Seif, ameiomba serikali iwape kibali kitakachowaruhusu kununua kahawa kwa wakulima kwa bei nzuri tofauti na ilivyo sasa.


COLLEGES & INSTITUTES CANADA | COLLÈGES & INSTITUTS CANADA
collegesinstitutes.ca | collegesinstituts.ca

## FINANCE AND ADMINISTRATIVE OFFICER POSITION - EMPOWERMENT THROUGH SKILLS PROGRAM (ESP)

Colleges and Institutes Canada (CICan) invites eligible candidates to indicate their interest in employment as a Finance and Administrative Officer to the Empowerment through Skills Program (ESP) in Tanzania, implemented by CICan in close collaboration with the Ministry of Education, Science and Technology (MOEST) through the Department of Technical and Vocational Training (DVET).
The individual Finance and Administrative Officer will be responsible for providing effective and efficient financial and administrative support to the ESP project office in Tanzania.

**Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:**

i. Superior written and spoken English and Swahili skills.
ii. Tanzanian citizen or legally permitted to work in Tanzania. Note: CICan will not provide a work permit or sponsor individuals.
iii. Recognized certificate, diploma, or degree in a related field (administration or business or finance or accounting).
iv. A minimum of 5 years' experience in a similar role with an international organization in financial and accounting processes, including, but not limited to, experience preparing financial claims and reports for programs, budgets, and reconciliations.
v. A minimum of 5 years' experience providing administrative and financial support in an office setting on international development projects with an international organization.
vi. Demonstrated ability using Microsoft Office Suite, especially Excel where advanced knowledge is expected.
vii. Experience organizing large meetings and events with international and government partners.
viii. Ability to prioritize and organize work effectively and efficiently under pressure and tight deadlines.
ix. A diligent work ethic and professional behavior.
x. Demonstrated experience working with an international team.

Interested candidates should send their applications electronically ONLY to **info@tz.collegesinstitutes.ca** no later than **26th September 2021.**

**The application should comprise of:**

- Curriculum Vitae (CV);
- Cover Letter;
- Copies of relevant certificates, permission to work in Tanzania; and
- Name, physical addresses, and contact details of three references who can comment on personal conduct and previous work done.

216466301



COLLEGES & INSTITUTES CANADA | COLLÈGES & INSTITUTS CANADA
collegesinstitutes.ca | collegesinstituts.ca

## DRIVER - EMPOWERMENT THROUGH SKILLS PROGRAM (ESP)

Colleges and Institutes Canada (CICan) invites eligible candidates to indicate their interest in employment as a Driver to the Empowerment through Skills Program (ESP) in Tanzania, implemented by CICan in close collaboration with the Ministry of Education, Science and Technology (MOEST) through the Department of Technical and Vocational Training (DVET).

The individual Driver will be responsible for providing effective and efficient driving and messenger support to the Senior Technical Advisors and ESP field office.

**Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:**

i. Fluency in English and Swahili.
ii. Tanzanian citizen or legally permitted to work in Tanzania. Note: CICan will not provide a work permit or sponsor individuals.
iii. Possession of a continuous driver's license and excellent driving record.
iv. A minimum of 5 years' experience in a similar role with an international organization.
v. A minimum of 5 years' experience driving safely and responsively in a professional setting, preference for experience with similar international development projects.
vi. Demonstrated ability in interacting effectively with program staff, staff of partner ministries, other government agencies, technical and vocational institutes, other partners, and stakeholders.
vii. Demonstrated ability to adjust to changing priorities and work with minimum supervision and attention to detail.
viii. A diligent work ethic and professional behavior.
ix. Demonstrated experience working with an international team.
x. Ability to work both independently and collaboratively on a team

Interested candidates should send their applications electronically ONLY to **info@tz.collegesinstitutes.ca** no later than **26th September 2021**.

**The application should comprise of:**

- Curriculum Vitae (CV);
- Copies of relevant certificates and/or driving license, permission to work in Tanzania; and
- name, physical addresses, and contact details of three references who can comment on personal conduct and previous work done.

216466301

# Manispaa Moro yaridhia gulio la nguo Machinga kila J'mosi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imeridhia kufanyika kwa mnada (Gulio) kila Jumamosi katika eneo la Soko Kuu la Chifu Kingalu ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara wadogo (Machinga) kujiongezea kipato.

Uamuzi wa kufanyika kwa mnada huo umekuja baada ya siku chache kupangwa upya na kukabidhiwa vibanda vya biashara eneo hilo na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro.

Meya wa Manispaa hiyo, Pascal Kihanga alisema hayo juzi katika mkutano ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, uliokuwa na jukumu la kuwapanga na kukabidhi vibanda vya kisasa vilivyojengwa eneo la Soko Kuu la Chifu Kingalu kwa matumizi ya wafanyabiashara hao.

Kihanga alisema, manispaa hiyo kwa kushirikiana na mkuu wa wilaya na viongozi wa wafanyabiashara wadogo wataendelea kutafuta maeneo mazuri na kuwapanga upya ili shughuli zao waziendeshe bila bughudha na staha nyakati zote bila kujali jua ama mvua. Alisema, baada ya kupangwa katika eneo la soko kuu hilo, manispaa imeridhia ombi lao la kufanyika kwa mnada wa nguo kila Jumamosi sokoni hapo kutoka eneo la kikundi ambalo si rafiki kutokana na ukosefu miundombinu bora hasa ya vyoo na maji.

Baadhi ya wafanyabiashara wakielezea kwa nyakati tofauti kuwapanga maeneo mazuri ya kufanya biashara, walimpongeza Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Rais kwa kuwawekea mazingira mazuri ya ufanyaji kazi wao bila kubughudhiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Msando alianza kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwapanga upya wafanyabiashara wadogo 788 maeneo ya kudumu ya kufanyia biadhara zao kwa utaratibu. Katika eneo la Soko Kuu la Chifu Kingalu, vibanda vimejengwa kwa kufuata mistari na kupewa majina ya viongozi wa kitaifa kiwamo Rais Samia, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na baadhi ya viongozi maarufu wa mkoa huo wakiwamo machifu.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kulia) na Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishangoma, wakizindua Bodi Mpya ya Wakurugenzi wa DAWASA iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rada zaleta neema ya mapato nchini

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imesema rada nne za kuongozea ndege zilizofungwa katika viwanja vinne vya ndege zimeisaidia kuongeza idadi ya ndege zinazotua na kuruka pamoja na mapato yatokanayo na tozo za kutumia anga la Tanzania.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipofanya ziara katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa ajili ya kukagua shughuli mbalimbali ikiwamo kuangalia rada ya kuongoza ndege inavyofanya kazi.

Alisema serikali imewekeza fedha nyingi kununua rada hizo ambazo zimefungwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Songwe na Mwanza na kwamba uwekezaji huo umeanza kuleta matunda.

Kadhalika alisema kwa sasa rada hizo zinasaidia kuona ndege zote zinazopita katika anga la Tanzania na zote zinalipa tozo za serikali.

Aliwapongeza vijana wa kitanzania wanaoongoza rada hizo na kwa sasa nchi inajiongoza yenyewe, badala ya kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi.

"Nimeenda Songwe, Dar es Salaam, Kilimanjaro na hapa Mwanza na kweli nimeona serikali ilivyofanya uwekezaji katika usafiri wa anga," alisema.

Waitara alisema rada hizo pia zimesaidia ulinzi wa nchi kwa kuwa zinaona kila kitu kinachokatiza katika anga la Tanzania. Kuhusu mapato, Waitara alisema yamepanda licha ya kuwapo ugonjwa wa Covid-19 katika nchi mbalimbali duniani.

Kwa upande wake, Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, Pascal Kalumbate, alisema sekta ya utalii kwa sasa imeimarika wanapokea ndege nyingi uwanjani hapo.

Pia kwa sasa ulinzi katika uwanja huo umeimarika kutokana na kufungwa mtambo huo unaofanyakazi saa 24 kwa siku.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**JOSEPH LEONARD KABOBOYE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 347 DMH.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **LIN/LIN/RB/452912/2021**

116468102



**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.39/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY THOMAS**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MERINA AMOS**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27/09/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 13/09/2021

116468602



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ZUBEDA BATISTA MHELELA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 517 BEL – SCANIA. CHASSIS NAMBA 5102244. ENGINE NAMBA 6021920.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MKB/TR/183/2021.**

116468502


# Tahadhari uagizaji majokofu, viyoyozi vya mitumba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amewataka Watanzania kutunza mazingira kwa kununua bidhaa rafiki zisizokuwa na kemikali zitokanazo na gesi haribifu zinazoweza kumong'onyoa tabaka la ozoni.

Jafo alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuhifadhi Tabaka la Ozoni.

Katika maadhimisho hayo Waziri Jafo, alifanya ziara ya kukagua maduka ya bidhaa za mitumba za viyoyozi na majokofu yanayotumia gesi haribifu na kusababisha kuharibu tabaka hilo. Katika ziara hiyo alitoa elimu kwa mafundi mchundo wanaojihusisha na uuzaji na utengenezaji wa bidhaa za mitumba ya majokofu pamoja na viyoyozi vinavyotumia gesi.

Alisema ozoni ni tabaka la hewa ambalo liko katika anga la juu la pili linalofahamika kitaalamu kama stratosphere ambalo linaweka aina ya tabaka ama tambara angani na kuzuia mionzi mikali ya jua inayoweza kuleta athari katika afya za binadamu na viumbe hai kuja moja kwa moja duniani.

Alisema uharibifu wa tabaka la ozoni unasababisha madhara mbalimbali duniani ikiwamo kuongezeka kwa kiwango cha joto pamoja na kuleta mabadiliko ya tabia ya nchi jambo ambalo ni hatari kwa afya ya binadamu na viumbe hai.

"Wafanyabishara wengi wamekuwa wakiuza majokofu ya mtumba yanayotumia gesi R22 na kuharibu mazingira... uzeni mitungi ya gesi kuanzia R200 na kuendelea," alisisitiza.

Alitoa wito kwa vijana wanaojishughulisha na masuala ya ufundi wa viyoyozi na majokofu ya mtumba kutumia aina ya gesi inayoruhusiwa na viwango vya kimataifa.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema Dodoma inakuwa kwa kasi na kwamba kuna haja ya kutengeneza jukwaa la pamoja litakalosaidia kutoa elimu kwa wananchi.

"Ni kweli wananchi wamekuwa wakinunua majokofu ya mtumba ambayo yameonekana kuwa na madhara na hiyo yote inatokana na kutokuwa na uelewa juu ya madhara hayo, lakini sasa kama tutakuwa na jukwaa la pamoja la kutoa elimu juu ya madhara ya bidhaa hizi za mtumba nina imani bidhaa hizo za mtumba hazitanunuliwa," alisisitiza Mwema.

Mmoja wa mafundi anayejishughulisha na ufundi wa viyoyozi vya mtumba, Matukuta Juma, alisema kutokana na ushauri huo watahamasisha wengine kutumia mitungi ya gesi inayokubalika na kuiomba serikali kuwapunguzia bei gesi ambayo haiharibu mazingira.

HABARI KITAIFA

# Bodi Pamba yakwama kukopesha pembejeo

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKURUGENZI wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Marco Mtunga, amesema kwa sasa mfuko huo hauna uwezo wa kugawa au kuwakopesha wakulima pembejeo kutokana na kukabiliwa na ukata.

Aliwataka wakulima katika msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2021/2022 kujiandaa kujinunulia pembejeo badala ya kuitegemea bodi hiyo.

Akieleza hali halisi na mwenendo wa zao hilo jana katika kikao cha wadau wa zao la pamba kilichofanyika mjini Bariadi mkoani Simiyu, Mtunga alisema uzalishaji wa pamba sio mzuri kwa kuwa unaendelea kushuka. Alisema sababu inayochangia tatizo hilo ni wakulima hao kutoelewa namna ya kupambana na kuua wadudu wanaoshambulia zao hilo na matokeo yake wanaishia kulalamikia mbegu na dawa kuwa siyo nzuri.

"Siyo siri zao la pamba uzalishaji wake haujawa mzuri ukilinganisha na miaka ya nyuma...wakulima wengi kwa muda mrefu wamekuwa hawaelewi namna ya kupambana na kuua wadudu kwenye pamba...wao wanajua mdudu ni yule anayeshambulia kitumba cha pamba na kusahau kuwa kuna funza wanaofyonza majani ya pamba na kuna aina nne ya wadudu waharibifu wa pamba," alisema Mtunga.

Aliongeza kuwa ingawa bodi imekuwa ikisaidia kutoa elimu juu ya suala hilo, maofisa ugani wanatakiwa kutoa elimu kuhakikisha suala hilo linafanyiwa kazi na kumsaidia mkulima kulima kilimo chenye tija.

Baadhi ya wadau wa pamba walishauri kampuni za pamba kupewa zabuni ya kusambaza pembejeo vijijini ili kila mkulima aweze kununua mapema.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alitoa wiki mbili kuhakikisha kampuni zitakazopewa kibali cha kusambaza pembejeo zianze kazi hizo.

Kafulila pia alikitaka Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Simiyu, (SIMCU), kubadilika katika mfumo wake wa kujiendesha ili kiwe maeneo ya uzalishaji kuliko kusubiri kukusanya pamba ya mkulima ambayo hawajui gharama zake na shida anayoipta mkulima.

# Wazalishaji watakiwa kusajili maeneo ya uzalishaji

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS wa Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Koyi Paul, amewataka wazalishaji na wafanyabiashara nchini kusajili maeneo yao ya uzalishaji, uuzaji, usambazaji na uhifadhi wa vyakula na vipodozi kama sheria inavyoelekeza ili kuepuka usumbufu.

Koyi alitoa mwito huo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya utoaji leseni na vyeti kwa wazalishaji 227 wakiwamo wakubwa, wa kati na wajasiriamali wadogo ambao bidhaa zao zimekidhi viwango vya kutumia alama ya bora ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Alisema ni wajibu wa wazalishaji na wafanyabiashara kuhakikisha wanatii sheria za nchi bila shuruti, hatua itakayowawezesha kuepukana na usumbufu kwenye shughuli zao.

Aidha, aliwataka wajasiriamali ambao bidhaa zao zimekidhi matakwa ya ubora kutumia fursa hiyo ipasavyo, kwa kuwa ili waweze kwendana na sera ya viwanda ni lazima wazalishe bidhaa zitakazoweza kushindana kwenye soko la ndani na nje ya nchi. Koyi alisema anatambua kwamba haikuwa kazi rahisi kwa wazalishaji hao 227 kupata vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora ya shirika hilo, hivyo ni matumaini yake kwamba mafanikio hayo yataongeza tija katika biashara na huduma wanazozitoa.

"Mtaenda kuwa mabalozi wazuri wa TBS, ili wazalishaji wengine waweze kuitikia wito wa nyayo zenu, lengo kuu likiwa ni kuwa na bidhaa bora na salama kwa ajili ya kulinda afya za walaji na kupanua wigo wa masoko kwa wazalishaji," alisema Koyi.

Alifafanua kwamba kwa mafanikio hayo anaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kulipia gharama za kuhudumia wajasiriamali katika ukaguzi na upimaji wa bidhaa zao.

Aliongeza kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu serikali imetumia Sh. milioni 715 kwa ajili ya kuwahudumia wajasiriamali wadogo na utaratibu wa kulipa wao wenyewe umewekwa kupitia Sera ya Madeni ya Shirika la TBS.

Alipongeza utaratibu uliowekwa na shirika hilo wa kuwafanyia tathmini wajasiriamali baada ya miaka mitatu ya kugharamiwa na serikali ili kujiridhisha na uwezo wao wa kujigharamia wenyewe.

"Kwa taarifa nilizonazo ikibainisha kuwa mjasiriamali husika hajapata uwezo huo serikali itaendelea kumgharamia," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, alisema leseni na vyeti 227 zimetolewa kwa wazalishaji ambao wamethibitisha bidhaa zao na kukidhi matakwa ya viwango kwa kipindi cha kuanzia Mei hadi Septemba, mwaka huu.

Alisema wazalishaji waliopata leseni na vyeti vya kutumia alama ya ubora wamegawanyika katika makundi matatu. Alitaja makundi hayo kuwa ni wazalishaji wakubwa, wakati pamoja na wajasiriamali wadogo.

Kwa mujibu wa Dk. Ngenya vyeti na leseni walizokabidhiwa zitasaidia bidhaa zilizothibitishwa katika maeneo mbalimbali ikiwamo kuongeza imani kwa umma juu ya ubora, kukubalika sokoni, kupata faida ya kiushindani sokoni na kuingia na kuuzwa katika soko la Afrika Mashariki pasipo kufanyiwa vipimo zaidi.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## TRAINING INSTITUTE

## KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Institute ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 18/10/2021. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/09/2021.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia (A,B,C,D)
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa au kusoma nchini.
vi. Asiwe na mchoro au tojo ( visible tattoo) kwenye sehemu za mwili zinazoonekana.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV
v. Kwa wageni, vibali vya kukaa au kusoma Tanzania

**Fomu ya Maombi ni bure.**
**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Institute**
**Box no 543**
**Dar Es Salaam.**
**Email , training@airtanzania.co.tz**

**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING INSTITUTE.**




PO Box 123456 / Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +254 20123456 / Fax +254 20123456 /email:info@airtanzania.com
website:www.airtanzania.com

216462101

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mahaba kwa mashabiki Simba, Yanga yasiishie siku ya tamasha

**KAMA** ilivyokuwa wakati Klabu ya Yanga inaadhimisha Siku ya Kilele cha Mwananchi Agosti 29, mwaka huu, kwa maelfu kujitokeza kwa wingi na kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa, ndivyo ilivyotokea kwa watani zao, Simba jana Septemba 19 kwenye tamasha lao la Simba Day, kwa dimba hilo kufurika.

Klabu hizo mbili zilitumia siku hizo tofauti kutambulisha wachezaji wake kuelekea msimu mpya wa 2021/22, pamoja na kuuza vifaa mbalimbali vya klabu hiyo zikiwamo jezi, lakini mashabiki wa soka kupata burudani ya muziki kutoka kwa wasanii mbalimbali.

Mbali na burudani na utambulisho huo, mashabiki wa soka pia walishuhudia mechi za timu zote tatu za klabu hiyo, kuanzia ile ya vijana wanawake hadi ya wakubwa kwa wanaume ambapo kwa Yanga, ilicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Zanaco ya Zambia wakati Simba ikikipiga na TP Mazembe ya DR Congo.

Hakika kwa matamasha yote mawili ya timu hizo, ilikuwa zaidi ya burudani kwa wanachama, mashabiki na wadau wa soka kwa ujumla, kwani walionyesha mahaba makubwa kwa kuhudhuria uwanjani hapo, na kwa namna ilivyokuwa hatutarajii kama kuna anayeweza kujutia kiingilio chake.

Ni wazi kwa maelfu yale ya mashabiki waliojitokeza, tunaona kuna jambo linahitajika kwa uongozi wa klabu hizo kutazama ni wapi wanapokosea katika kuwahamasisha mashabiki wao kuendelea kuonyesha mahaba kwa kuhudhuria kwa wingi uwanjani kila timu zao zinapocheza.

Kwa namna ambavyo tumekuwa tukifuatilia matamasha hayo, tumebaini mbali na mechi ama utambulisho wa wachezaji unaofanywa siku hizo, uwapo wa burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali, huchangia kwa kiasi kikubwa kuwavutia mashabiki wa rika zote wanawake kwa wanaume kuhudhuria uwanjani.

Hivyo, uongozi wa klabu hizi kongwe nchini na zenye mashabiki wengi nje na ndani ya nchi, kuna haja ya kutazama namna nyingine ya kuwavutia mashabiki wa soka wa jinsia zote kwenda uwanjani, ili kutunisha vipato vyao hasa ukizingatia udhamini unaotolewa bado haukidhi kwao katika kujiendesha.


Na hilo halipaswi kuwa kwa Simba na Yanga pekee, bali klabu zingine zinapaswa kutumia mfano huo katika kubuni mbinu mbadala za kuwavutia mashabiki kuhudhuria viwanjani kwa wingi badala ya kutegemea tu wachache wenye mahaba na mechi. Kwa namna matamasha hayo mawili yalivyofana kwa kuhudhuriwa na mashabiki wengi, ni wazi ipo haja sasa klabu za soka nchini kujaribu kujumuisha baadhi ya wasanii kutoa burudani kabla ya mechi pengine kunaweza kuchangia kuvutia mashabiki wa jinsia zote kuhudhuria kwa wingi viwanjani na kuzifanya siku za mechi hususan za mwishoni mwa wiki kuwa sehemu ya 'mtoko' kwa familia mbalimbali.

Tunaamini endapo katika mechi za klabu hizo na nyingine nchini, zitahudhuriwa na angalau robo tatu ama nusu ya mashabiki kama waliojitokeza Simba Day Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na Agosti 29 kwenye Kilele cha Siku ya Mwananchi, klabu hizo zinaweza kujiendesha kisasa kabisa kwa mapato ya mlangoni na kufanya makubwa zaidi kitaifa na kimataifa.

Nipashe tukiwa wadau wakubwa wa sekta ya michezo nchini, tunatamani kuona hamasa ya mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani ikiendelea na si tu kwa Simba na Yanga pekee, bali kwa klabu zote, kwani kwa kufanya hivyo kutalitangaza soka letu na hata kuvutia wachezaji wengi bora zaidi kutoka nje ya nchi kuja kucheza nchini, lakini pia wawekezaji wakubwa.

Tunatamani kuona ligi yetu ikitoka katika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika na kukwea juu zaidi, hivyo mashabiki wanapaswa kutambua kwamba wana mchango mkubwa katika hilo kwa upande wa mahudhurio yao uwanjani. Kwa mantiki hiyo, itapendeza zaidi kama msimu huu mpya wa 2021/22 wataufanya kuwa tofauti kabisa kwa mahudhurio kuongezeka viwanjani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Azam, Biashara zisibweteke kimataifa

**KAZI** bado ni ngumu kwa timu za soka za Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, licha ya kushinda mechi zao za awali. Nazizungumzia timu za Azam na Biashara United ambazo zinashiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF).

Tumeona, Azam imefanikiwa kutinga raundi ya kwanza kwa kuitoa Horseed ya Somalia kwa jumla ya mabao 4-1, kwenye mechi ya kwanza,

Uwanja wa Azam Complex, ilishinda mabao 3-1, Septemba 11 kabla ya juzi, Jumamosi kufunga timu hiyo bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. Ni mechi ambayo ilitakiwa ichezwe nchini Somalia. Lakini kutokana na kutokuwa na usalama wa uhakika kwenye nchi hiyo, ikachezwa hapa hapa Tanzania.

Ina maana mechi zote mbili za Azam imezicheza nyumbani kwa tafsiri nyingine. Hii ni bahati kwa timu hiyo ya Tanzania.

Kwa upande wa Biashara United nayo ilipata ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Dikhil ya Djibouti, halafu ikashinda mabao 2-0 hapa nyumbani kwenye Uwanja wa Azam Complex

Tuanze na Azam, pamoja na kucheza mechi zote nyumbani, ukweli ni kwanza imepata ushindi wake kwa tabu tofauti na jinsi wengi walivyodhani.

Kwa usajili uliofanywa wa klabu hiyo mwaka huu, haikutarajiwa kama Azam ingepata ugumu kuifunga Horseed, ilitegemewa ingeshinda kirahisi zaidi tofauti na ilivyoshinda. Hata kwenye mechi ya kwanza ambayo ilishinda mabao 3-1, ilianza kushtukizwa kufungwa, ndipo wachezaji walipojua jukumu lao ambalo walipashwa kulifanya.

Ni kweli Horseed ina wachezaji ambao wana vipaji vya kuuchezea mpira miguuni, lakini walikuwa wanakosa vitu vingi ambavyo Azam ilitakiwa kwenye mechi ya kwanza iitandike mabao mengi tu.

Kwenye mechi ya marudiano, Horseed walionekana hawana tena hofu yoyote. Walicheza kama wako kwao nchini Somalia, sipati picha kama wangekuwa kwao, hivyo Azam kupata bao moja kwa tabu.

Sasa Azam inakwenda kukutana na Pyramids ya nchini Misri. Ni mechi ngumu mno na inabidi sasa ijipange kisawasawa, la sivyo itakuwa imefunguliwa mlango wa kutokea, wachezaji wasibweteke na ushindi dhidi ya Horseed ambao hata hivyo Watanzania wengi hawakuridhika nao.

Si matokeo wala uchezaji, Azam ikumbuke inakwenda kucheza na timu iliyofika nusu fainali ya kombe hilo la shirikisho msimu uliopita na kutolewa kwa mikwaju ya penalti 5-4 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco baada ya suluhu ya bila kufungana nyumbani na ugenini. Raja Casablanca ndiyo waliokwenda kuchukua ubingwa huo. Hapo utapata picha kuwa Azam inakwenda kukutana na timu ya aina gani.

Hakuna tofauti kubwa kati ya ilichokifanya Azam na Biashara United. Dikhil siyo timu mbaya sana, lakini pia si timu nzuri. Biashara United imesonga mbele kwa jumla ya mabao 3-0, ikishinda bao 1-0 ugenini na mabao 2-0 nyumbani.

Kocha Patrick Okumu itabidi awaongezee vijana wake mbinu na uwezo, kwani inakwenda kucheza na timu yenye uwezo mkubwa zaidi mara tatu au nne kuliko Dikhil.

Biashara itacheza na mshindi kati ya Hay Al Wadi ya Sudan na Al Ahli SC ya Libya. Pamoja na kwamba si timu maarufu, lakini zinatoka kwenye nchi ambazo ziko vizuri kisoka, hivyo itegemee ushindani mkali tofauti na ule ilioupata kwa Dikhil.

Kwa maana hiyo, ni kwamba Azam na Biashara sasa ndio zimeingia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, hizi mechi za nyuma zilikuwa ni mechi za mchujo, au ni kama dibaji tu, lakini michuano yenyewe ndiyo inaanzia hapa.

Kwa jinsi tulivyoziona mechi zao, bado zinatakiwa zikaze msuli na zina kazi ngumu kuipeperusha bendera ya Tanzania na kuzilinda nafasi nne ilizonazo.

Kinachotakiwa ni maandalizi ya uhakika ili kufanikisha malengo, zisibweteke kwa ushindi wa mechi zao zilizopita. Zikumbuke kuwa michuano ya kombe hilo ina mechi nyingi mpaka kutinga makundi, tofauti na Ligi ya Mabingwa Afrika. Kwa sababu hata kama zikipita hapo, zitalazimika kusubiri timu zitakazotolewa kwenye Ligi ya Mabingwa kucheza mtoano ili kutinga makundi.

Ni safari ndefu yenye milima, mabonde na miiba, lakini ninakumbushana tu kwamba siku zote michuano ya kimataifa huwa ni migumu tofauti na inavyofikiriwa, kila hatua inayopigwa ndipo mbele kunakuwa kugumu zaidi.

# Wakulima wa ufuta waingiza bil. 120/-

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKULIMA wa ufuta mkoani Lindi wamepata Sh. bilioni 120.6 baada ya kuuza kilo 49,885,228 za zao hilo kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa na Mshauri wa Kilimo na Rasilimali Watu, Majid Myao, wakati akiwasilisha taarifa ya mauzo ya zao hilo katika mkutano uliowakutanisha wadau wa zao hilo.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Myao alisema Mkoa wa Lindi uliweka malengo ya kuzalisha kilo 68,500,000 za ufuta, lakini kutokana na hali ya hewa kutokuwa nzuri na idadi ya ukubwa wa mashamba wamekusanya kilo 49,885,228 sawa na asilimia 72.8, hivyo kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa.

Myao alisema mauzo na makusanyo ya ufuta huo ni kupitia minada 16 iliyofanywa na vyama vikuu vya ushirika vya Runali na Lindi Mwambao.

Alisema kutokana na kipato hicho, Sh.bilioni 8.8 ni makato ya ushuru yaliyopelekwa kwa wadau mbalimbali zikiwamo halmashauri za wilaya na manispaa kupitia mifuko ya elimu, kilimo, tari.

Myao alisema pia katika mgao huo Sh. bilioni 3.6 ni ushuru wa halmashauri zote sita ambazo ni Kilwa, Lindi Manispaa, Nachingwea, Mtama, Ruangwa na Liwale, wakati Sh. bilioni 1.2 zikipelekwa katika mfuko wa elimu ngazi ya wilaya na mkoa ukipatiwa mgao wa Sh. milioni 99.7 kila mmoja.

Alisema ugani na PYT Center ulipewa mgao wa Sh. milioni 99.7, Tari Sh. milioni 49.8, vyama vya msingi Sh. bilioni 2.9 wakati Sh.milioni 748.2 zikikadhiwa kwa vyama vikuu vya ushirika na Sh. bilioni 113.838 zimelipwa kwa wakulima.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Rajabu Telak, akizungumza na wadau hao wa kilimo, aliwasisitiza kutumia fedha walizolipwa kujiletea maendeleo, kwa kujenga bora na kusomesha watoto.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule, akizindua kitabu cha Maisha Halisi ya Mtoto wa Mtaani, kilichoandikwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya James, James Yustar (kushoto), katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mtangazaji wa Clouds Media, Dk. Isack Maro. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Daraja lanusuru vifo vya wananchi

**Na Neema Sawaka,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Mwabayanda, Kata ya Old-Shinyanga katika Manispaa ya Shinyanga wameondokana na tatizo la watu kupoteza maisha kutokana na kusombwa na maji pamoja na mifugo yao baada ya kukamilika kwa daraja la Bubiki lililoko mkoani Shinyanga. Mradi huo ambao umejengwa kwa kiwango cha lami umegharimu kiasi cha Sh. milioni 958. Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), mkoani Shinyanga, Mibara Ndirimbi, alipokagua barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 1.6.

Ndirimbi alisema barabara hiyo ujenzi wake upo katika hatua za mwisho na kwamba muda wowote watakabidhiwa ili isaidie kuondoa shida ya usafiri pamoja na watu kupoteza maisha kwa kusombwa na maji. "Barabara hii ya Shinyanga Bubiki iliyojengwa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 1.6 kwa kujumlisha matengenezo madogo ya daraja na karavati imegharimu Sh. 958,450,000 na itawanufaisha wakazi wote wa mkoa huo na nje ya mkoa watapita katika barabara hii," alisema Ndirimbi.

# 'Walimu wasiachiwe jukumu la wanafunzi pekee'

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KAIMU Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Edwin Kayuwi, amewataka wazazi kujenga tabia ya kukagua maendeleo ya wanafunzi badala ya kuwaachia walimu pekee.

Kayuwi alitoa wito huo juzi aliposhiriki mahafali katika Shule ya Msingi Mtakativu Alfonsa, Chalinze mkoani Pwani.

Alisema ili kukuza ufaulu kwa wanafunzi ni lazima wazazi wajenge tabia ya kukagua daftari za watoto wao wanaporejea nyumbani, wawape muda wa kujisomea na kupumzika wawapo nyumbani.

"Ili shule zetu za Chalinze ziongoze kwenye kufaulisha ni lazima wazazi wabadilike na kushirikiana na walimu kufuatilia maendeleo ya watoto wetu," alisema.

Alisema kutokana na shule za binafsi kutegemea ada za wazazi ni vyema wakawa na utaratibu wa kulipa kwa wakati ili mipango inayopangwa itekelezeke kwa wakati.

Pia, alisema shule za serikali wanafunzi hawalipi ada kutokana na kila kitu kufanywa na serikali na za binafsi ambazo wazazi wanalipa ada wanatakiwa kufanya kama walivyokubaliana ili walimu wapate mishahara kwa wakati na shule zifanye maboresho mengine.

Alisisitiza kila shule kuwa na utaratibu wa chakula ili wanafunzi wafanye vizuri kwenye masomo.

Alisema Halmashauri ya Chalinze inaanza mkakati wa ufuatiliaji kwa shule zote na kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula shuleni kwa kufuata maelekezo ya serikali.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Rosbin Mathew, alisema shule hiyo ilianzishwa 2012 ikiwa na wanafunzi wanane na sasa wamefikia 349.

Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, Melkisedeki Komba, alisema wanafunzi pia wanafundishwa maisha ya uraiani na kuwa na maadili kwa jamii.

Komba pia aliwasihi wanafunzi kujiandaa kwa masomo ya ngazi za juu na kufanya vizuri kwa kuwa mfano mzuri kwenye hatua zinazofuata kutokana na waliyofundishwa shuleni.

# TRA yatupiwa zigo matengenezo EFD

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA) imeombwa kusaidia kuzifanyia matengenezo mashine za kielektroniki (EFD) zinazotumika kukusanyia taarifa za mauzo zinapoharibika, ili kuwapunguzia mzigo mkubwa wafanyabiashara pale zinapoharibika.

Ombi hilo limetolewa na wafanyabiashara mbalimbali wa Manispaa ya Lindi, wakati wa kikao na watendaji wa TRA.

Kikao hicho kilichokuwa chini ya Kaimu Meneja wa TRA Mkoa wa Lindi, Beatricial Kahoho, kilikuwa na lengo la kuwajulisha mabadiliko ya sheria mpya ya kodi, zinazotumiwa na mamlaka hiyo katika ukusanyaji na usimamizi wa maduhuli ya serikali.

Hoja hiyo ilitokana na wafanyabiashara hao kutaka kufahamu mmiliki halali wa EFD kati ya wafanyabiashara na TRA na kujibiwa ni mali halali ya serikali katika kuhakikisha mapato yake hayapotei.

Wafanyabiashara hao walisema kwa vile EFD zinazotumika kukusanyia mapato ni mali ya serikali, ni vizuri TRA ikabeba jukumu la kuzitengeneza zinapoharibika ili kuwapunguzia mzigo mkubwa wa kutozwa fedha nyingi. Awali akiwasilisha mada katika kikao hicho, mkadiriaji mkuu wa kodi ma Dar es Salaam, James Robert Mtalika, alisema lengo la mabadiliko ya vifungu mbalimbali vya sheria yanalenga kudhibiti uvujaji mapato ya serikali na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa maduhuli.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya wafanyabiashara mkoani Lindi, Hamisi Abdallah Livembe, alipongeza hatua zinazochukuliwa na TRA katika kuwapatia elimu, kwani itawasaidia kupata uelewa wa kufahamu mambo mengi.



Wafanyakazi wa Benki ya Exim Tanzania wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Mikopo, Zainab Nungu (katikati), wakifanya usafi kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi jirani na Hospitali ya Ocean Road jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Usafi Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aagiza wanafunzi wazururaji kukamatwa

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MKUU wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa wilaya hiyo, kuwakamata vijana wanaotakiwa kuwa shule lakini wanazagaa mitaani kufanya shughuli nyingine.

Meja Gowele alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga mkutano wa wadau wa elimu uliofanyika Utete katika wilaya hiyo.

Aliagiza wazazi na walezi wa vijana hao kukamatwa ili kukomesha utoro kwa wanafunzi unaochangia wilaya hiyo kuwa na ufaulu hafifu.

Alisema kwa sasa kunahitajika kwa na mabadiliko katika wilaya hiyo kuinua kiwango cha elimu kwa watoto, pia kudhibiti mambo yanasababisha kuwa na ufaulu duni kwenye mitihani ya kitaifa.

Alitoa onyo kwa wazazi kuwatumia watoto wao kama kitega uchumi cha familia na chanzo cha mapato.

"Tumepata taarifa wapo watoto wanalea familia huku wanasoma hii inachangia kuwa na ufaulu duni, wengine wanaozeshwa wakiwa na umri mdogo ili wazazi wapate fedha, nasema hawa sio kitega uchumi cha familia hatua zitachukuliwa kwa atakayebainika," alisisitiza Mkuu huyo wa wilaya.

Pia, alipiga marufuku wazazi wanaomaliza kesi za mimba kifamilia na kuanzia sasa hatua zitachukuliwa kutokana kesi hizo kutakiwa kuendeshwa kisheria kukomesha vitendo hivyo.

Alisema ili kupambana na ufaulu duni katika wilaya hiyo viongozi wa wilaya watafanya ziara itakayolenga kuongea na wazazi na walezi ili kukomesha tabia ya utoro na kusisitiza wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto badala ya kuwaachia walimu.

Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Rufiji, Zainabu Abdallah, alisema vipo vikwazo wanakabiliana navyo katika idara yake ambavyo ni pamoja na ukosefu wa hosteli kwa wasichana na wavulana ambao unaelezwa kuwa chanzo cha utoro, kuchelewa vipindi na mimba za utotoni kutokana na umbali mrefu wanaotembea.

Kikwazo kingine alikitaja kuwa ni uchakavu wa majengo hususani katika shule za Mkongo na Utete, upungufu wa mabweni zenye kidato cha tano na sita pamoja na ukosefu wa chombo cha usafiri hasa gari ili kurahisisha utendaji wa kazi.

## RC Mwanza ahamasisha chanjo ya corona mtaani

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amelazimika kuingia mtaani kuhamasisha wananchi kuchanja chanjo ya UVIKO-19, ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona ulioikumba dunia.

Akizungumza na wananchi wa Buhongwa na Mwalo wa Butuja mkoani humo, wilayani ya Ilemela, alisema ni wakati wa wananchi hao kuchanja chanjo ya Covid-19 na kuachana na imani potofu zinazoenezwa katika mitandao.

Aliongeza kuwa moja ya mkakati wa serikali ni kuhamasisha wananchi juu ya masuala ya maendeleo na utoaji elimu juu ya chanjo ya UVIKO-19 ili wananchi wawe na afya njema.

"Hii simu ukiitumia vizuri inakupeleka mbinguni ukiitumia vibaya utajinyonga na kuingia jehanamu naomba mtambue kuwa kila jambo kuna wataalamu wake waliobobea, hivyo tuwasikilize wataalamu wa afya, ugonjwa huu hauchagui rangi upo na unaua," alisema Gabriel.

Alisema ili kuboresha afya na kuokoa maisha yao, wapate chanjo hiyo na wataalamu wa afya watakuwa katika maeneo hayo kuwapatia huduma hiyo kwa kuwa Rais Samia alipoona vifo vya Watanzania vinaongezeka alileta chanjo ili kuwanusuru na virusi hivyo.

"Dunia imevurugika hivyo sipendi na wewe uvurugikiwe kila mtu lazima awe salama na asiwapo mwananchi wa mkoa huu apoteze maisha kwa uzembe kwa sababu tu hajapata chanjo, nawaomba mjitokeze kwa wingi wataalamu wapo hapa mtumie hiyo fursa kujihakikishia usalama wa afya zenu," alieleza Gabriel.

Aliwataka wananchi kutoogopa chanjo hiyo kwa sababu haina shida na ndiyo njia sahihi duniani kwa sasa kwa kuwa kuna baadhi ya mambo hayawezi kufanyika bila kuchanja.

HABARI KITAIFA

## Wanafunzi waonywa ngono, matumizi ya dawa za kulevya

**Na Marco Maduhu**, SHINYANGA

WANAFUNZI wa shule za sekondari mkoani Shinyanga, wameonywa kutojiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Pia wamepewa angalizo la kufanya ngono katika umri mdogo, bali wajikite kwenye masomo, ili watimize ndoto zao na kuwa tegemeo katika familia na taifa kwa ujumla.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, ambaye pia ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, alibainisha hayo juzi wakati akitoa msaada wa kompyuta tano na printa moja, katika Shule ya Sekondari Ngokolo Mjini humo.

Alisema vijana wengi wamekuwa wakizima ndoto zao kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, huku wanafunzi wa kike wakiambulia ujauzito na kuacha masomo, na kuwataka wanafunzi mkoani Shinyanga wasijiingize kwenye vitendo hivyo vibaya, bali wazingatie masomo yao.

"Hivi karibuni tulikuwa na operesheni ya dawa za kulevya jijini Tanga na Arusha, tumeshuhudia vijana wengi wamepoteza ndoto zao, kuna wengine nilisoma nao chuoni, nao wameathirika na dawa hizo, naombeni sana wanafunzi zingatieni masomo yenu msijiingize huko mtapotea," alisema Katambi.

"Leo nimegawa kompyuta na printa katika Shule hii ya Sekondari Ngokolo, pia nimetoa vitabu 324 vya masomo ya sayansi katika shule nne za sekondari Manispaa ya Shinyanga kila shule vitabu 81, lengo langu nataka nyie wanafunzi mpende kusoma masomo ya sayansi ili tupate wataalamu ndani ya nchi," aliongeza.

Naye mmoja wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari Ngokolo, Chausiku Mrisho, ambaye anasoma kombi ya sayansi, walimpongeza Katambi kwa kusapoti suala la elimu, huku wakiahidi kusoma kwa bidii ili kutimiza ndoto zao.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo, Malale Sawaka, alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,240, walimu 37, masomo ya Sayansi wapo wanane, uhitaji walimu 12, na kufanya kuwa na upungufu wa walimu wa wanne na kuiomba serikali iwapatie walimu hao, ili kusiwapo upungufu huo.

# Kampeni kuongeza uzalishaji wa korosho

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuunga mkono kampeni ya kuchochea uzalishaji zaidi wa korosho kwa wakulima wa mikoa ya Lindi na Mtwara.

Kampeni ya "Vuna zaidi na NBC Shambani" imezinduliwa na Benki ya NBC maalum kwa wakulima wa zao la korosho katika mikoa hiyo, huku serikali ikiahidi kuunga mkono na kuutumia mkakati huo katika kufanikisha adhma yake ya kuzalisha tani 700,000 za zao hilo kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo iliyofanyika mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa zao hilo wakiwamo viongozi wa kiserikali, viongozi vyama vya msingi (AMCOS) na vyama vikuu vya ushirika, Mkuu wa mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema mkakati huo umekuja wakati mwafaka kipindi ambacho serikali imejipanga kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka matarajio ya tani 280,000 ya mwaka huu hadi tani 700,000 ifikapo mwaka 2025.

"Ni wazi kwamba NBC Shambani imekuja eneo sahihi kwa wakati sahihi! Serikali ilipojiwekea lengo la kuzalisha tani 700,000 ilifahamu fika kwamba kitovu cha kufanikisha adhma hiyo kipo Mtwara. Imekuwa vema zaidi benki ya NBC imeliona hili pia na sisi wana Mtwara tunawahakikishia kwamba tupo tayari kuupokea mpango huu kwa kuwa umekuja kutushika mkono. Rai yangu kwa wana Mtwara naomba tuipokee NBC Shambani ili kwa pamoja tufanikishe hili," alisema Gaguti.

Aidha, Brigedia Jenerali Gaguti alilisisitiza suala zima la nidhamu ya fedha miongoni mwa wakulima wa zao hilo, huku akitoa wito kwa viongozi vyama vya msingi (AMCOS). vyama vikuu vya ushirika na wakulima kwa ujumla kutumia vema mafunzo yanayotolewa na benki hiyo kuhusu umuhimu wa kujiwekea akiba, matumizi ya bima mbalimbali ikiwamo bima ya afya pamoja na kuwekeza kwenye zana za kisasa za kilimo.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema kampeni hiyo ya miezi mitatu ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kujizatiti kwenye kuinua kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwamo zao la korosho kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara.

"Tunashukuru kuona kwamba adhma yetu hii tayari imepokelewa vyema na walengwa ambao ni wakulima na hiyo ndio sababu hadi leo hii tunapozindua kampeni hii ya NBC Shambani tayari zaidi ya AMCOS 40 na wakulima wa korosho zaidi 11,000 wamejiunga na huduma hii. Tunashukuru kwa mapokeo haya na kupitia kampeni hii pamoja na kutoa zawadi mbalimbali tutaendelea kutoa elimu na hamasa kwa wakulima zaidi ili tufikie malengo yetu kwa pamoja," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na wakulima kutoka Benki ya NBC, Raymond Urassa, alisema kupitia kampeni hiyo wakulima wa zao hilo wataweza kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa na zawadi za kifamilia kama kanga, mabegi na madaftari.

"Kwa upande wa AMCOS vinaweza kujishindia zawadi kubwa zaidi ikiwamo maguta (Toyo) pamoja na matrekta. Ili walengwa hawa wote waweze kujishindia zawadi hizi wanatakiwa wafungue akaunti benki ya NBC na wapitishe fedha za malipo yao kwenye akaunti hizo na moja kwa moja watakuwa wameingia kwenye droo ya kujishindia zawadi hizi," alifafanua.

Viongozi wa AMCOS katika mkoa huo Salum Ngumbo na Habiba Kambutu walisema mpango huo umekuwa na tija kubwa kwa wakulima, huku wakionyesha kuvutiwa zaidi na suala la kutokuwapo kwa makato ya fedha zao pindi wanapopitisha fedha hizo kupitia akaunti zao za NBC Shambani.




Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti (katikati), akijaribu ubora wa moja ya matrekta ambayo ni miongoni mwa zawadi zitakazotolewa kwa washindi wa kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' mahususi kwa wakulima wa korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi, katika uzinduzi wa kampeni hiyo mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni viongozi waandamizi wa Benki ya NBC; Mkurugenzi Mtendaji, Theobald Sabi (kulia) na Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo, Elibariki Masuke (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gari la kwanza kupita daraja la Selander Desemba

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amesema ujenzi wa daraja jipya la Selander lililoko jijini Dar es Salaam lenye urefu wa km. 1.03 na upana wa mita 20.5 ujenzi wake umefikia asilimia 93, kwamba jaribio la magari kupita litaanza Desemba mwaka huu.

Daraja hilo lenye barabara unganishi zenye urefu wa km 5.2 linajengwa na Kampuni ya GS Engineering ya Korea, litakalopita baharini kuanzia ufukwe wa Coco Beach (Oysterbay) kwenda Hospitali ya Aga Khan (Maeneo ya Ocean Road).

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa maendeleo ya mradi huo, Waziri Mbarawa alisema hadi sasa mradi huo umefikia asilimia 93 na kwa sasa mkandarasi anaendelea na ujenzi wa sehemu ya juu ya daraja baada ya kukamilisha ujenzi wa sehemu ya chini kwa asilimia 100 ikiwamo, nguzo za msingi 254, vitako vyake 16 pamoja na nguzo 16 za juu za daraja.

"Mkandarasi amekamilisha kujenga km 1.026 kati ya km 1.030 sawa na asilimia 99.7 na kuweka nyaya za daraja 30 kati ya 30 sawa na asilimia 100," alisema Prof. Mbarawa.

Aliongeza kwa upande wa barabara unganishi mkandarasi anaendelea na kazi za kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Barack Obama, Toure na barabara mpya zenye upana sawa na ule wa daraja.

Aidha, akiwa katika ukaguzi huo Profesa Mbarawa aliridhishwa na ushirikishwaji wa wazawa kwenye mradi kwa ajili ya mafunzo ambapo jumla ya wafanyakazi 773 kati ya hao wafanyakazi 704 ni wazawa sawa na asilimia 91.

"Nimefurahishwa sana kukuta wataalamu wanaojenga mradi huu ni Watanzania na ninategemea mafunzo haya yatasaidia kujenga uwezo na ujuzi utakaosaidia Taifa letu baadae," alisema Prof. Mbarawa.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, akiwasilisha taarifa ya mradi alimweleza Waziri Mbarawa kwamba kazi zinazoendelea kwa sasa upande wa barabara ni ujenzi wa tabaka la mwisho la lami, ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua pamoja na uwekaji nguzo za taa na misingi yake pamoja na usimikaji wa taa za barabarani.

Mhandisi Mativila aliongeza kuwa wanatarajia ifikapo mwishoni mwa Desemba mwaka huu kazi ndogo ndogo zitakuwa zimekamilika na kuanza kupitisha magari kwa majaribio.

Prof. Mbarawa yupo katika ziara ya kikazi jijini Dar es Salaam ambapo amekagua ujenzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya wizara yake ikiwamo upanuzi wa gati namba moja hadi saba katika Bandari ya Dar es Salaam, upanuzi wa Barabara ya Kimara hadi Kibaha, ujenzi wa Daraja jipya la Selander pamoja na Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka (BRT) awamu ya pili.

# GGML yaelekezwa jinsi ya kusaidia saratani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAKAMU Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambaye ni Mbunge wa Manonga, Igunga, Seif Gulamali, ameitaka Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kusaidia Hospitali ya Kanda ya Ziwa Bugando vifaa vya matibabu ya ugonjwa wa saratani kwa wanawake.

Gulamali alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya nne ya teknolojia na uwekezaji kwenye sekta ya madini Mkoa wa Geita.

Alisema kutokana na madhara makubwa yanayotokana na uchimbaji wa dhahabu kupitia zebaki, kuna madhara makubwa ambayo yanasababisha kutokea kwa ugonjwa wa saratani kwa jamii hasa kutokana na maji kutitirika hadi kuingia kwenye kwenye mito, visima na mabwawa pamoja na maeneo mbalimbali na kwenye vyakula hivyo kusababisha madhara hasa saratani.

Aidha, aliitaka GGML kusaidia sekta ya afya kwa kuboresha huduma za afya kwenye ugonjwa wa saratani, wadau wakubwa wa maendeleo waweze kuchangia katika kuboresha katika huduma za ugonjwa wa salatani kwa sababu wangonjwa wengi wa salaratani wa Kanda ya Ziwa wanapata huduma hiyo katika Hospitali ya Ocean Road Dar es Salaam ambapo ni mbali pmoja na gharama.

Alisema huduma ya ugonjwa wa saratani ikisogezwa karibu itawaondolea wagonjwa wa saratani usumbufu wa kwenda kupata huduma hiyo Dar es Salaam.

"Tumeona Hospitali ya Bugando wako kwenye hatua ya kuboresha huduma hiyo ya saratani...GGML isaidie hospitali hiyo au kama inaona huko ni mbali basi waboreshe Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita ili waweze kusaidia na kupunguza usumbufu wa wagonjwa wa saratani kwenda kupata huduma hiyo Dar es Salaam ambako ni mbali.

Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Elisha, Maya, alisema lengo la maonyesho hayo kwa Mkoa wa Geita ni kubadilishana uzoefu kwa wachimbaji wakubwa wa madini kwa kuwapa uzoefu wachimbaji wadogo.

Maya alisema lengo lingine ni kuhakikisha sekta ya huduma ya kifedha kuwapatia mikopo nafuu wachimbaji wadogo wa madini kwa kuwapatia mikopo ndiyo maana beki zote zimekwenda kwenye uwanja wa maonyesho kwa ajili hiyo.

Meneja wa GGML, Manase Ndoroma, alisema ombi la Kamati ya Bunge amelichukua na atalifikisha kwenye uongozi wa GGML.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (watatu kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel (kulia), pamoja Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati) wakiwa na Spika wa Bunge mstaafu, Anna Makinda (wapili kulia) na viongozi wengine wakishangilia makabidhiano ya vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 10 vilivyotolewa na Benki ya NMB, jana kwa ajili ya vituo vya afya vya Hogoro na Sejeli wilayani Kongwa, mkoani Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu 100 wapewa miguu bandia

**Na Romana Mallya**

WATU 100 wenye ulemavu wameanza kutembea tena, baada ya Kampuni ya Kamal ya jijini Dar es Salaam kuwapatia miguu bandia ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za maendeleo na kujikwamua kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika Mkoa wa Pwani, alisema mkoani humo kuna zaidi ya watu 130,000 wenye ulemavu ambao wanahitaji huduma ya miguu bandia.

"Jengeni utamaduni wa kupenda kufanya kazi badala ya kuwaachia

Watanzania wenzenu wanaotoka mikoa mingine kuja kushika nafasi mbalimbali za kazi katika viwanda vinavyowekeza katika mkoa huu. Vijana wengi wa Mkoa wa Pwani hawapendi kufanya kazi.

"Ninapata malalamiko ya mara kwa mara kutoka kwa wawekezaji wanaohoji ni kwa nini watu wa Mkoa wa Pwani hupenda kutoa udhuru mara kwa mara wawapo kazini? Utasikia leo anaenda kuzika na kesho kuna ngoma. Lazima tubadilike," alisema.

Kunenge alisema Katiba inamruhusu kila raia kuishi sehemu yoyote nchini ili mradi asivunje sheria na kuwataka wakazi wa Mkoa wa Pwani kutokuwa watazamaji wenzao wanapopambana kufanya kazi.

Alisema tayari kampuni ya Kamal inatekeleza mpango wa kuwawezesha wajasiriamali wa Watanzania kumiliki viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho ambapo kwa kuanzia, watu zaidi ya 100 watamiliki viwanda hivyo vinavyojengwa katika eneo maalum la viwanda mkoani humo.

Alisema alipendekeza kama viwanda hivyo vitamilikiwa kwa kiasi kikubwa na wakazi wa mkoa huo na kuwahamasisha wachangamkie fursa hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Issa, alisema hivi sasa wilayani hapo kuna jumla ya viwanda 145 vyenye ukubwa tofauti na kusisitiza kuwa serikali itafanya kila linalowezekana kuweka mazingira sawa kwa wawekezaji kufanya kazi bila vikwazo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kamal Group, Sameer Gupta, alisema kampuni yake hutoa msaada wa miguu bandia kupitia taasisi yake ili kuwawezesha wenye ulemavu waendelee kufanya majukumu yao ya kujipatia riziki kama ilivyokuwa mwanzo kabla hawajapata ulemavu.

Alisema hadi sasa jumla ya miguu bandia 1000 imeshatolewa na kampuni hiyo kusaidia wenye ulemavu nchini.

Alisema mbali na miguu bandia, kampuni hiyo pia inatoa chakula kwa zaidi ya wanafunzi 3,500 wanaosoma katika shule za msingi za Chanika, Dar es Salaam na Nzasa ya Bagamoyo kwa muda wa miaka saba hadi hivi sasa ambapo taarifa zinaonyesha utoro umepungua kwa kiasi kikubwa.

# Pinda aitaka Shinyanga kujitathmini kiuchumi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameutaka Mkoa wa Shinyanga kufanya tathmini ya maendeleo ya kiuchumi ili uweze kupiga hatua kwa kutumia rasilimali zake.

Rasilimali zilizoko mkoani humo ni mifugo, mazao ya pamba na tumbaku pamoja na madini ya dhahabu na almasi.

Alibainisha hayo juzi mkoani Shinyanga alipozungumza na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo, kabla ya uzinduzi wa mashindano ya michezo ya umoja wa vijana wa chama hicho, UVCCM GREEN CUP katika uwanja wa michezo wa CCM Kambarage.

Alisema mkoa wa Shinyanga una rasilimali nyingi ambazo zinaweza kuukuza kiuchumi, lakini hazitumiki ipasavyo na kuuomba uongozi wa mkoa huo kufanya tathmini ya maendeleo ya kiuchumi.

Aidha, alisema unatakiwa kuitishwa mkutano mkubwa ili kupata mawazo ya wadau mbalimbali na kuubadilisha mkoa huo.

"Mkoa huu wa Shinyanga una rasilimali nyingi sana na ndiyo maana kipindi changu nilipokuwa bado Waziri Mkuu, tulianzisha hapa viwanda vingi vikiwamo vya kuchambua pamba na kutengeneza mafuta ya kula kwa kutumia malighafi pamba... hii ndiyo namna ya kutumia rasilimali zenu kuwaletea maendeleo," alisema Pinda.

"Hivyo nawaombeni sana viongozi wa mkoa huu pamoja na chama, mfanye tathmini ya maendeleo ya kiuchumi pamoja na kuitisha mkutano mkubwa wa kiuchumi ili na mimi niwepo niwasaidie namna ya kutumia rasilimali zenu kuinuka kiuchumi," alisisitiza Pinda.

Katika hatua nyingine, alitaka CCM mkoani Shinyanga, kuwatumia vijana ndani ya chama hicho kuhakikisha wanapanda miti ya kutosha mkoani humo, ili kuufanya uwe wa kijani na kuendana na falsafa yao.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alimshukuru Pinda kwa kuwapatia busara zake na kuahidi kuufanyia kazi ushauri wake ili kuubadilisha mkoa huo kiuchumi.

Naye Mwenyekiti wa CCM mkoani humo, Mabala Mlolwa, alimshukuru Pinda kwa kuendelea kuwa karibu na wananchi wa Shinyanga tangu alipokuwa madarakani hadi sasa.

# Nipashe Spotika




11 BORA YENYE THAMANI KUBWA EPL KWA SASA UK. 12 - 13




RONALDO

# USAJILI MPYA ULIOFUNGUA MSIMU HUU KWA KUTUPIA

**LONDON,** England

HUKU athari za kifedha kutokana na janga la COVID-19, zikianza kupungua, klabu nyingi zilizimua kuingia sokoni kwa nguvu kipindi hiki cha majira ya joto. Ingawa mikataba ya mkopo ilibaki kuwa njia inayopendelewa ya biashara kwa klabu nyingi, kuna ambazo hazikusita kutumia fedha nyingi kuimarisha vikosi vyao.

Wachezaji wengi mashuhuri, pamoja na Cristiano Ronaldo, Lionel Messi, Romelu Lukaku na Sergio Ramos, walibadilisha klabu msimu huu.

Kwenye makala haya, hapa tunaangalia wachezaji watano bora ambao walifunga kwa mara yao ya kwanza kwenye klabu zao mpya msimu huu, wafahamu sasa...

### #5. EDIN DZEKO (INTER MILAN)

Edin Dzeko ni mmoja wa wachezaji wachache waliofunga mabao 50 katika ligi tatu kati ya ligi tano kubwa Ulaya Ulaya.

Baada ya misimu michache ya kwanza yenye matunda kwenye Ligi Kuu Italia akiwa na AS Roma, mshambuliaji huyo wa Bosnia & Herzegovina alikuwa hitaji la ziada pale kwenye Uwanja wa Olimpico. Lakini mabingwa wa Serie A wanaotawala, Inter Milan hivi karibuni walikuja kupiga simu na kupata huduma yake.

Licha ya kutimiza umri wa miaka 35, mapema mwaka huu, Dzeko alithibitisha thamani yake kwa kutengeneza mwangaza mzuri kwa 'Nerazzurri' hao. Alifunga na kutoa asisti katika ushindi wa mabao 4-0 wa Inter dhidi ya Genoa katika mchezo wao wa ufunguzi wa Serie A msimu huu. Mechi hiyo ilikuwa ya 200 kwa Dzeko kwenye Ligi Kuu Italia.

Mshambuliaji huyo mkongwe amefunga mara 86 na kutoa asisti 40 katika michezo 202 ya Serie A. Dzeko aliifungia Bosnia & Herzegovina katika sare yao ya 2-2 na Kazakhstan katika mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia 2022.

### #4. ACHRAF HAKIMI (PSG)

Achraf Hakimi ni mmoja wa walinzi bora ambao wana uwezo mkubwa wa kufunga. Baada ya kujipatia jina kule Borussia Dortmund, kijana huyo mwenye umri wa miaka 22, akang'ara zaidi katika msimu wake mmoja kule Italia, msimu uliopita.

Hakimi alifunga mara saba na pia kutoa asisti kumi wakati Inter Milan ikishinda taji la Ligi Kuu kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka kumi. Lakini kwa sababu za kifedha, 'Nerazzurri' hao walilazimika kumuuza Hakimi baada ya msimu mmoja tu. Vigogo wa Ligue 1, PSG hivi walimnyakua nyota huyo wa kimataifa wa Morocco kwa euro milioni 60.

Beki huyo wa kulia akifunga bao kwenye Ligue 1 wakati PSG ikishinda 2-1 dhidi ya Troyes. Katika mchakato huo, alikuwa mchezaji wa kwanza wa PSG katika miaka miwili kufunga kwenye mechi yake ya kwanza Ligi Kuu Ufaransa.

### #3. EDUARDO CAMAVINGA (REAL MADRID)

Eduardo Camavinga ni mmoja wa viungo vijana wa kusisimua zaidi kwenye mchezo huo kwa sasa.

Kijana huyo alinyakuliwa na Real Madrid siku ya mwisho ya uhamisho. Camavinga alianza kucheza pale Santiago Bernabeu, akifunga ndani ya dakika tano tu kwenye mechi yake ya kwanza ya Real Madrid wakati wakishinda mabao 5-2 nyumbani dhidi ya Celta Vigo.

Camavinga alikuwa mmoja wa wafungaji wachanga zaidi kwa Ufaransa wakati alipofunga kwenye ushindi wa mabao 7-1 dhidi ya Ukraine mwaka jana.

### #2. ROMELU LUKAKU (CHELSEA)

Romelu Lukaku ni mmoja wa washambuliaji wakali katika mchezo huo kwa sasa. Amekuja Chelsea baada ya msimu mzuri na Inter Milan. Msimu wake wa mwisho, Lukaku alikuwa mchezaji wa kwanza kwa zaidi ya miongo miwili kufunga mabao 20 na kutoa asisti kumi wakati 'Nerazzurri' hao wakishinda Scudetto yao ya kwanza katika miaka 10.

Chelsea walikuja wakitaka huduma yake, wakimnyakua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa uhamisho wa euro milioni 115. Lukaku alitua Uwanja wa Stamford Bridge, akifunga bao lake la pili kwa klabu, katika ushindi wa 2-0 wa Ligi Kuu dhidi ya Arsenal.

Mechi mbili baadaye, Mbelgiji huyo alifunga bao, mabao yake ya kwanza huko Stamford Bridge tangu aachane na klabu hiyo karibu miaka kumi iliyopita. Kuwasili kwa Lukaku kumeongeza makali kwenye safu ya ushambuliaji ya Chelsea, kitu ambacho kilikosekana sana kwa washindi hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

### #1. CRISTIANO RONALDO (MANCHESTER UNITED)

Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wachezaji bora kuuboresha mchezo huu. Wakati wa kazi nzuri, karibu ya miaka miwili, amepata malengo na kushinda mataji mengi.

Baada ya kurudi Manchester United msimu huu wa majira ya joto, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 hakuchukua muda mwingi kuanza. Alifunga bao katika mchezo wake wa kwanza kwa klabu hiyo baada ya miaka 12 wakati United iliifunga Newcastle United 4-1.

Siku chache baadaye, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, alifunga na kuweka rekodi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kufikisha mabao 135. Lakini ushujaa wake haukutosha kwani United ilikubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Young Boys.

## ISIKUPITE

HILI ni tamasha (Simba Day) la 13 tangu kuanzishwa kwake na klabu hiyo mwaka 2009, na katika mechi 12 za kirafiki ilizocheza siku hiyo, ukiacha ya jana dhidi ya TP Mazembe, Simba imeshinda mechi 7, sare 2 na kupoteza 3 (1-0 Villa, 0-0 Express, 0-1 Victors, 1-3 Nairobi Stars, 4-1 Villa, 0-3 Zesco, 1-0 Villa, 4-0 Leopards, 1-0 Rayon, 1-1 Asante Kotoko, 3-1 Power Dynamos, 6-0 Vital'O, ... vs TP Mazembe?



Extra Time

# 11 BORA YENYE THAMANI KUBWA EPL KWA SASA


ROMELU LUKAKU

**LONDON,** England

KATIKA misimu michache iliyopita, Ligi Kuu England imeibuka kama ligi ya mpira wa miguu yenye usawa zaidi na iliyopangwa zaidi barani Ulaya. **Huku Real Madrid na Barcelona wakipata mwenendo mbaya zaidi kwa upande wa Ulaya na vile vile katika utendaji wao wa ndani, klabu za Uingereza zimeanzisha ukuu wao.**

Kutokana na miaka mingi ya kutawala kwa Hispania, mashabiki wa Ligi Kuu England walifarijika kuona mapenzi ya Kiingereza katika mechi mbili kati ya tatu za mwisho za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa kutumia jumla ya karibu euro bilioni tatu, klabu za Uingereza zilikuwa vikifanya kazi sana katika kipindi cha uhamisho wa msimu wa majira ya joto wa 2021. Licha ya mapambano yao ya hivi karibuni, Arsenal ilimaliza kipindi cha uhamisho kama watumiaji wakubwa zaidi, ikimleta mchezaji kama Ben White na Albert Lokonga.

Kwingineko, Liverpool na Tottenham walifanikiwa kuimarisha chaguo zao za beki wa kati kwa kuwasajili Ibrahima Konate na Cristian Romero. Baada ya ubashiri mwingi, Leon Bailey mwishowe alijiunga na Ligi Kuu England, akisaini kule Aston Villa kama mbadala wa moja kwa moja wa Jack Grealish aliyetua Manchester City.

Romelu Lukaku, Bryan Gil, Patson Daka, Marc Cucurella na mashine ya kufunga mabao Cristiano Ronaldo ni moja wapo ya nyongeza maarufu kwa wachezaji bora wa Uingereza msimu huu.

Kuzingatia mabadiliko mengi, klabu zilipata mabadiliko makubwa katika hesabu zao. Wakati pande za LaLiga na Serie A zilipoteza wachezaji nyota wengi. Ligi Kuu England ilitawala zaidi kwa kupata vipaji bora.

Kama matokeo, mgawanyiko wa kwanza wa mpira wa miguu wa Kiingereza unaweza kujivunia seti ya wachezaji wenye nyota nyingi kote Ulaya. Kwa nukuu ya jumla ya euro milioni 955, ngoja tuangalie wachezaji 11 wenye thamani zaidi kwa sasa, twende sasa...

### KIPA: ALISSON BECKER (EURO MIL. 60, LIVERPOOL)

Amesimama kwa urefu wa futi 6.3, Alisson Becker ndiye golikipa mwenye thamani zaidi Ligi ya England. Nambari moja hiyo ya Brazil ilinunuliwa na Jurgen Klopp mwaka 2018 kwa euro milioni 62.5, na kumfanya kuwa kipa ghali zaidi ulimwenguni kwa kipindi kifupi.

Alisson alithibitisha kuwa mtu muhimu zaidi kwa Klopp, akiibadilisha Liverpool kuwa miamba barani Ulaya. Baada ya kusajili 'Wekundu' hao walishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu.

### BEKI WA KULIA: TRENT ALEXANDER-ARNOLD (EURO MIL. 75, LIVERPOOL)

Kuinuka kwa umaarufu wa Trent Alexander-Arnold kumekuwa kama kwa kushtukiza. Mwingereza huyu mwenye umri wa miaka 22, mwanzoni alitumiwa kama beki msaidizi wakati wa kutokuwapo kwa Nathaniel Clyne, ambaye alikuwa anapambana na majeraha wakati huo.

Lakini kiwango chake cha kushangaza na uthabiti, haraka kikamfanya kupewa nafasi ya beki wa kulia na Klopp. Akiwa na hali ya kipekee ya ubunifu, Alexander-Arnold ni mmoja wa mabeki bora zaidi wa kulia barani Ulaya kwa sasa.

### BEKI WA KATI: RAPHAEL VARANE (EURO MIL. 70, MANCHESTER UNITED)

Upotezaji wa Real Madrid ulionekana kuwa faida ya Manchester United wakati 'Mashetani Wekundu' hao walipotumia fursa ya kumsajili beki wao nyota, Raphael Varane mara tu alipopatikana.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia, amewasili Old Trafford baada ya kukaa miaka 10 na miamba hiyo ya Hispania.

### MLINZI WA KATI: RUBEN DIAS (EURO MIL. 75, MANCHESTER CITY)

Nyongeza nyingine ya hivi karibuni kwenye Ligi Kuu, ni mwaka mmoja tu umepita tangu Ruben Dias ajiunge na Manchester City kwa kitita cha Euro milioni 68. Lakini tayari mlinzi huyo wa Ureno ameonyesha thamani zaidi.

Dias mwenye umri wa miaka 24, alinyakua tuzo ya mchezaji bora wa msimu wa Ligi Kuu wakati Man City iliponyakua taji lao la tatu la ligi ndani ya miaka minne.

### BEKI WA KUSHOTO: ANDREW ROBERTSON (EURO MIL. 65, LIVERPOOL)

Sehemu nyingine nzuri ya biashara iliyofanywa na Jurgen Klopp, Andy Robertson alijiunga na Liverpool mwaka 2017 kwa ada ya euro milioni tisa. Beki huyo wa pembeni mwenye umri wa miaka 27, alionyesha dalili za kuahidi kwa kushinda tuzo ya nyota wa mchezo katika mchezo wake wa kwanza na 'Wekundu' hao.

Baada ya kucheza kama msaidizi wa Alberto Moreno katika msimu wake wa kwanza, Robertson hivi karibuni aliiweka nafasi ya beki wa kushoto kuwa yake mwenyewe kwa kufanya kazi kwa bidii na uthabiti. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland amesaidia sana kufanikiwa kwa Liverpool.

### KIUNGO WA KATI: BRUNO FERNANDES (EURO MIL. 90, MANCHESTER UNITED)

Bruno Fernandes ameibadilisha kabisa Manchester United. Fernandes alikuwa na ushawishi wa haraka kwa wachezaji wa United. Wakati wa kusainiwa kwake kwa euro milioni 63 ilionekana kuwa kamari hatari sana.

Lakini Fernandes ameishi kwenye Ligi Kuu kama bata katika maji, akifunga na kutengeneza nafasi za kiwango cha dunia mara kwa mara. Baada ya mwaka mmoja na nusu tu, mchezaji huyo wa Ureno anachukuliwa kama mmoja wa nyota muhimu zaidi pale Old Trafford.

### KIUNGO WA KATI: KEVIN DE BRUYNE (EURO MIL. 100M, MANCHESTER CITY)

Anachukuliwa kama mchezaji bora kwenye Ligi Kuu England kwa muda mrefu sasa, Kevin De Bruyne bila shaka ni kipaji cha kizazi hiki. Mbelgiji huyo mbunifu ni hodari sana katika kuunganisha mchezo.

Alirudi Ligi Kuu England mwaka 2015 na kutua hapo Man City, akiwa amecheza mwanzoni kule Chelsea. De Bruyne hajaangalia tena nyuma tangu wakati huo, akicheza mechi zaidi ya 263 kwa Man City.

### KIUNGO WA KULIA: MOHAMED SALAH (EURO MIL. 100M, LIVERPOOL)

Mohamed Salah ameichukua Ligi Kuu England miguuni mwake tangu alipotua Liverpool mwaka 2017. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Misri, alijiunga na timu ya Liverpool chini ya Jurgen Klopp kwa ada ya euro milioni 42.

Lakini Salah amelipa fadhila kwa kufunga mabao 127 katika mechi 206. Msimu wa 2017-18 alifunga mabao 32 kwenye ligi hiyo.

### KIUNGO WA KUSHOTO: JADON SANCHO (EURO MIL. 100M, MANCHESTER UNITED)

Jadon Sancho ni hodari katika kucheza upande wa kushoto. Mshambuliaji huyo hodari alinunuliwa na Manchester United msimu huu wa majira ya joto baada ya sakata la uhamisho wa muda mrefu uliopita kwa misimu mingi. Wakati milioni 85 inachukuliwa kuwa bei ya biashara, kipaji chake ni muhimu zaidi.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, amekuwa ufunuo tangu alipoonekana kuwa muhimu zaidi kule Borussia Dortmund.

### MSHAMBULIAJI: ROMELU LUKAKU (EURO MIL. 100, CHELSEA)

Romelu Lukaku hivi karibuni alirudi kwenye Ligi Kuu England na kutua Chelsea katika moja ya uhamisho wa ghali zaidi. Baada ya kurudisha sifa yake kule Inter Milan kutokana na misimu miwili ya kutisha Serie A, mshambuliaji huyo wa Ubelgiji alihamia Stamford Bridge kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 115.

Huku mabao 116 ya Ligi Kuu yakiwa tayari chini ya mkanda wake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ana muda wa kutosha kuingia katika kumi bora ya orodha ya wafungaji wa mabao ya wakati wote. Mshambuliaji huyo wa Chelsea amekuwa na mwanzo mzuri wa maisha wakati wa kurudi Stamford Bridge, akiwa na mabao matatu katika mechi mbili.

### MSHAMBULIAJI: HARRY KANE (EURO MIL. 120, TOTTENHAM)

Mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England, Harry Kane amekuwa na Tottenham kwa muda mrefu. Nahodha huyo wa Uingereza ni gwiji wa Ligi Kuu England aliye na mabao 166 katika mechi 248 tu. Takwimu hii inamweka nafasi ya saba katika chati za ufungaji wa wakati wote.

Anachukuliwa kama mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi cha sasa, Kane bado hajashinda taji lolote. Hivi karibuni alihusishwa na uhamisho wa fedha nyingi kwenda Manchester City, lakini hakuna kitu kilichotekelezeka. Kwa hivyo, nahodha huyo wa England amebaki Tottenham na atakuwa na lengo la kuwasaidia kumaliza katika nne bora msimu huu.

## Nukuu

"Licha ya elimu yangu ya darasa la saba, lakini kwenye utawala wangu Simba SC, nilianzisha Simba Day, ambayo leo klabu inapata mpaka milioni 600, pia kufanya malipo ya kwanza ya Uwanja wa Bunju, kuanzishwa kwa Simba B na Simba Queens na kubeba ubingwa bila kufungwa," **Mwenyeti wa zamani wa Klabu ya Simba, Hassan Dalali.**



"Iliniuma sana kuwasha TV na kutoiona Arsenal ikicheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ulikuwa uchungu mkubwa, sitaki kukaa hapa na kutazama Arsenal tukiwa nje ya mashindano [haya]," **Kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta.**



"Mara zote ni vizuri kuwa uwanjani kusikia wimbo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mbele ya watazamaji, hakika ni hisia nzuri sana," **Mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski.**



Nipashe
Spotika

# NDOLANGA: NYOTA ILIYOZIMIKA NA MISIMAMO ISIYOYUMBISHWA



**Na Adam Fungamwango**

"NAIKUMBUKA ile kesi, hakimu alinyanyuka kwenye kiti, karani akamwambia bado hujamaliza kutoa hukumu. Hakimu akarudi kwenye kiti, akaniambia sina hatia, niko huru naweza kuondoka. Sikutaka kujua nini kitaendelea, niliondoka bila kugeuka nyuma." Yalikuwa ni maneno ya Muhidini Ndolanga aliyoyazungumza mwaka jana, juu ya kesi mbalimbali ambazo zilikuwa zinamkabili akiwa Mwenyekiti wa Chama cha Soka nchini Tanzania wakati huo kikiitwa (FAT), sasa (TFF).

Ndolanga, Mwenyekiti wa zamani wa chama hicho cha soka, kuanzia mwaka 1992, hadi 2004, hatunaye tena, alifariki dunia juzi kwenye Hospitali ya TMJ baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Ndolanga aliyezaliwa mwaka 1940, alifariki dunia akiwa na miaka 71, akiwa mmoja wa viongozi wa soka walioliongoza soka la Tanzania kwa muda mrefu zaidi.

### KAIONGOZA FAT MIAKA 12

Aliiongoza FAT kuanzia mwaka 1992, akichukua nafasi ya Mohamed Musa na kudumu madarakani kwa miaka 12 hadi 2004, alipoingia Leodgar Tenga ambaye ndiye aliyefanya mabadiliko na kukifanya chama hicho kuwa shirikisho na kuitwa, Shirikisho la Soka nchini (TFF).

Ndolanga anashika nafasi ya pili kwa kuliongoza soka la Tanzania kwa muda mrefu.

Kiongozi aliyedumu kwa muda madarakani kwenye soka la Tanzania ni Said El Maamry ambaye alifariki Julai mwaka huu.

El Maamry alikaa madarakani kwa miaka 13, kuanzia mwaka 1974, akichukua nafasi ya Ally Chambuso hadi 1987, alipoingia Mohamed Musa, hivyo kumzidi Ndolanga kwa mwaka mmoja zaidi.

### MISIMAMO MIKALI ISIYOYUMBA

Marehemu Ndolanga alipambana na mambo mengi, ikiwamo mkakati wa kutaka kumwondoa madarakani, lakini alisimama kidete na hakutetereka hadi alipoondoka mwaka 2004.

Nadhani kwenye utawala wake, ndiyo kulikuwa na migogoro mingi ya uongozi, kuliko kipindi kingine chochote kwenye utawala wa soka nchini.

Katika mahojiano yake mwaka jana, anasema hakumbuki mwaka gani, lakini alisema alishtakiwa kwa matumizi mabaya ya fedha.

"Serikali ndiyo ilinishtaki, niliambiwa nilitumia fedha za FAT vibaya, nakumbuka nilitumia kulipia simu yangu. Mwanasheria wangu akawaambia kuwa nilichofanya mteja wake ni sahihi kwa sababu nililipia huduma ya simu iliyotumika kwa kazi za kiofisi na ushahidi uliokuwapo wa mawasiliano yangu kutoka FAT kwenda Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Zurich, Uswisi," alisema wakati wa uhai wake.

Akaongeza kuwa wakati wa utawala wake mara kadhaa Serikali iliingilia masuala ya soka, ikiwa ni pamoja na kumwengua madarakani, lakini FIFA waliingilia kati na kutishia kuivua Tanzania uanachama, akarejeshwa.

### KUIBURUZA BMT MAHAKAMANI

Haukuishia hapo, ndani ya miaka yake ya utawala, aliwahi kuliburuza Baraza la Michezo ya Taifa (BMT) lililokuwa chini ya Mwenyekiti wake, Said El Maamry, mahakamani.

"Jina langu liliondolewa na BMT kwenye orodha ya wagombea FAT, nikaamua kuwashirikisha FIFA, wakaniuliza kama nina uhakika wa kushinda kesi, nikawajibu ndiyo na kweli nikashinda. Nikaibwaga tena serikali mahakamani, hapo ndipo nikabatizwa jina la Tyson," anasema kwenye mahojiano mwaka jana akifananishwa na bondia aliyekuwa kwenye kiwango cha juu wakati huo duniani, Mike Tyson.

### MWANACHAMA WA PAN AFRICAN

Ndolanga alikuwa mwanachama wa klabu ya Pan African, ambayo ilianzishwa mwaka 1976, kutokana na mpasuko wa uongozi na wachezaji kutoka Yanga, ambao walijiengua na kuunda klabu hiyo.

Aliingia madarakani kwaka 1992, kwenye uchaguzi uliofanyika Kibaha mkoani Pwani na aliongoza kwa misimamo mikali, akisimamia alichokiamini bila kuyumbishwa, lakini bila kuonekana na chembe chembe za kuibeba timu yoyote ile.

### HISTORIA YA MAISHA YAKE

Alizaliwa Septemba 23, 1940 Kijiji cha Nkunya wilayani Newala na kuanza elimu yake ya msingi kijijini Kitangiri Newala, hadi daraja la nne na kisha kujiunga na shule ya kati kuanzia darasa la tano hadi la nane Kijiji cha Mahuta.

Ndolanga alikuwa mwanafunzi pekee aliyefaulu Ukanda wa Kusini ukihusisha maeneo ya Tunduru, Mtwara, Lindi, Songea na Masasi, hivyo kupata nafasi ya kujiunga na Shule ya Sekondari, Tabora Boys mwaka 1957. Alipomaliza elimu yake alijiunga na Idara ya Wanyama Pori mwaka 1962, akipandishwa ngazi mbalimbali hadi kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyama Pori Novemba 1995 kwa mujibu wa sheria baada ya kutimiza miaka 55.

**JE, WAJUA?**



ALAN Shearer anaendelea kushikilia rekodi ya kuwa mchezaji aliyefikisha mabao 100 haraka zaidi kwenye Ligi Kuu England, akifikisha idadi hiyo baada ya mechi 124, akifuatiwa na Harry Kane (141), Sergio Aguero (147), Thierry Henry (160) na Mohamed Salah (162).



# Majaliwa kufungua kongamano uwezeshaji wanawake

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika kongamano la kitaifa la uwezeshaji wanawake kiuchumi lililopangwa kufanyika Oktoba 4, mwaka huu jijini Dodoma.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, akizungumza na waandishi wa habari, alisema kongamano hilo litawakutanisha wanawake kutoka mikoa mbalimbali na kuwataka wajitokeze kwa wingi.

Alisema kila taasisi zote za serikali na zisizo za serikali zinapaswa kushiriki katika kongamano la sita la uwezeshaji kiuchumi.

"Kongamano hili ni la tofauti na makongamano yaliyopita kimtazamo kwa sababu hili la safari hii limeboreshwa zaidi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa kongamano hilo, Suleiman Malela, alisema maandalizi yanaendelea vizuri hivyo washiriki wanapaswa kujiandaa ili kuja kuona namna ya uwezeshaji kiuchumi inavyofanyika.

Alisema kongamano la safari ni la aina yake, hivyo washiriki hawapaswi kukosa kushiriki na lengo lao ni kuona kongamano hilo linafanikiwa na wananchi wanashiriki kikamilifu.

Kwa upande wake, Husna Husein alisema wao kama wananchi wanasubiri kongamano hilo kwa hamu kubwa ili kukutana na wataalamu ambao watawaeleza namna ya uwezeshaji uchumi unavyokuwa.

"Tunawashukuru NEEC kufanya kongamano hilo kila mwaka tunahitaji kuona tunasonga mbele katia masuala ya kiuchumi," alisema.

# Sababu uharibifu mazingira wilayani Kongwa zaanikwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema madhara makubwa ya uharibifu wa mazingira katika Wilaya ya Kongwa yamechangiwa na kukithiri kwa shughuli za kibinadamu.

Kufuatia hali hiyo, amewataka wakazi wa wilaya hiyo kuweka msukumo kwenye agenda ya mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti na kutoharibu vyanzo vya maji.

Waziri Jafo aliyasema hayo juzi katika ziara yake ya siku moja wilayani humo ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Alisema Kongwa ya sasa si sawa na ya zamani kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu ikiwamo ukataji wa miti kwa matumizi ya kuni na mkaa.

"Mfano shamba la kilimo la Suguta pale zamani hali yake ilikuwaje leo nenda kaangalie hali ikoje? Ukienda Mlali angalia juu kwenye milima kule mwanzo ilikuwaje, Tubugwe, Chamkoroma, Suguta juu kule mbele milima ya Kongwa, leo hii hali ikoje? Ndio maana madhara ya uharibifu wa mazingira ni makubwa kwa Wilaya ya Kongwa."

"Madaraja yanayojengwa baada ya miaka mitatu yanatafuta pakupitia maji yanatengeneza mto mwingine wa kupita, maeneo mengi ukienda madaraja yametelekezwa kwa sababu ya maporomoko ya maji ni makubwa, athari za mazingira tusipolinda madaraja kama la Ibwaga pale hakuna kitu," alisema.

Alisema madaraja mengine yamehama kutokana na uharibifu wa mazingira miti imekatwa huku maeneo mengine yakiwa na mito mipya ambayo zamani haikuwapo.

"Shule ya Chamkoroma ilihamishwa kwasababu ya mto, mwanzo hakukuwa na mto, lakini kwasasa mto ni mkubwa kweli kweli hadi shule imehamishwa imejengwa eneo jingine, athari ni kubwa, angalia mabonde yaliyokuwa yanalima nyanya na miwa mwanzo umaarufu wa kilimo cha nyanya Kongwa umekufa, maeneo yamejaa mchanga, mito imeondoa kila kitu, rutuba imeondoka yote ni mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Alisema kampeni ya kukijanisha Dodoma ni endelevu, na Kongwa ni sehemu ya Mkoa wa Dodoma hivyo wapande miti kwa wingi na kuzingatia kilimo cha korosho kama zao la kimkakati.

Jafo alisema ajenda ya mazingira iende sambamba na upandaji wa miti kwa kila kaya walau miti mitatu ikiwamo ya kivuli na matunda ili jamii inufaike nayo na kunusuru miundombinu ya barabara na madaraja.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, alisema wilaya ya yake inaendelea kuhamasisha jamii kutambua umuhimu wa kutunza mazingira ikiwemo kutokata miti, kutoharibu vyanzo vya maji, kutovamia misitu, kupanda miti na kuhifadhi visiki asili.

Alisema takribani visiki hai 1,470,252 vimeainishwa na kutunzwa katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akiangalia bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali kinamama wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma katika banda la maonyesho, alipofika kufungua kongamano la maendeleo wilayani humo, lililofanyika mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waganga wakuu wapewa jukumu vifo vya wanawake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAGANGA Wakuu wa Mikoa na Halmashauri wameshauri kufanyike utafiti ili kubaini vikwazo vinavyokwamisha jitihada za kupunguza vifo vya kinamama na watoto na kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki katika risala yao iliyosomwa na mwenyekiti wao, ambaye ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita, Dk. Japhet Simeo, kwenye mkutano wa waganga hao uliofanyika kwa siku tatu jijini hapa.

Alisema kuna kasi ndogo ya kupungua kwa vifo hivyo vitokanavyo na uzazi ambapo kwa miaka mitatu mfululizo vimepungua kutoka vifo 1,744 mwaka 2018 hadi kufikia 1,614 mwaka 2020.

"Kiwango hiki cha vifo vilivyopungua ni kidogo ukilinganisha na matarajio yanayotokana na uwekezaji katika sekta ya afya, tunapendekeza kufanyike tafiti za kubaini changamoto na kuweka mikakati," alisema.

Hata hivyo, alisema kasi ya ongezeko la miundombinu kwenye sekta ya afya haiendani na uwekezaji katika bidhaa za afya kama vile dawa, vifaa tiba, vifaa na vitendanishi.

"Upatikanaji hafifu wa bidhaa za afya kutoka Bohari ya Dawa (MSD) suala hili limeathiri upatikanaji wa bidhaa za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya hususan hospitali za rufani za mikoa ambazo asilimia 50 ya fedha wanazokusanya hupelekwa bohari na kutopatikana na 'OS note' kwa wakati," alisema.

Mwenyekiti huyo alipendekeza kuwapo na bajeti ya vifaa tiba na dawa kwa ajili ya miundombinu ya kutolea huduma za afya iliyoongezeka na MSD izingatie matakwa ya utoaji wa 'OS note'.

Kuhusu chanjo ya UVIKO-19, alisema waganga hao wanashauri Wizara ya Afya iangalie uwezekano wa kuifanya kuwa ya lazima kwa watu wote wenye vigezo vya kuchanjwa na halmashauri ziwezeshwe kifedha ili kuendeleza mapambano ya Uviko-19 kwa ufanisi.

Kadhalika, alishauri kuwa na mpango wa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu hasa halmashauri za pembezoni ili kusaidia kupunguza wimbi la watumishi kuhamia maeneo mengine ya mijini.





# Ndoa ya dhana bado yawa kikwazo kwa wenzi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

IMEELEZWA kuwa idadi kubwa ya watu wanaoishi kwenye 'dhana za ndoa' hukosa sifa ya kupata mirathi na haki nyingine kama mwanandoa.

Hii ni kwa sababu ili iwe ndoa halali, lazima waishi sio chini ya miaka miwili na kuendelea na ithibitishwe na mahakama.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa Kifungu cha 160, ili kuwa mwanandoa walau wafikishe miaka miwili na wawe wameishi chini ya paa moja kwa muda wote huo.

Akizungumza na Nipashe wakati wa utoaji wa elimu ya msaada wa kisheria kwa wakazi wa Kijiji cha Kikota wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, Mkurugenzi wa Sauti ya Haki Tanzania, Laetitia Petro, alisema miongoni mwa athari za kuishi kwenye dhana ya ndoa ni kukosa sifa ya kupata talaka pale mmoja anapotaka kuachana na mwenzi wake, kwa sababu mahakama haina uthibitisho wa cheti cha ndoa.

"Wapo watu wanaishi kwenye dhana ya ndoa kwa zaidi ya miaka 20 bila kufunga ndoa, mmoja wapo akiamua kuolewa na mtu mwingine sheria inamruhusu kwa sababu yuko huru, vilevile linapokuja suala la mirathi sheria ya ndoa haimtambui aliyekuwa kwenye dhana ya ndoa kuwa msimamizi wa mirathi, lakini pia watoto wake hukosa sifa ya kupata mirathi," alisema Petro.

Aliwashauri wanawake kuwashawishi waume zao kufunga ndoa kama kweli wanapendana ili kulindana na kupata haki za msingi ikiwamo usimamizi wa mali, mwanaume kuwa na mamlaka ya kumchukulia hatua mkewe anapomfumania sambamba na kupata sifa ya kukopesheka kwenye taasisi za kifedha.

Mwanasheria wa Taasisi ya Tanzania Network of Legal Aid Providers (TANLAP), Kassile Kassile, alisema watu wengi wanakosa haki zao za msingi kwa sababu ya kutozifahamu sheria.

Alisema kupitia mradi wa Mwanamke Imara wanatoa mafunzo kwa wananchi wa mikoa ya Mbeya, Njombe na Kilimanjaro huku ukitekelezwa na mashirika mengine kama WLAC, ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Alisema watu wengi hukosa haki za msingi kwa sababu ya kutozifahamu sheria au kukosa wasaidizi wa kuwasaidia, hivyo mradi huo unalenga kuona haki inatendeka kwa kuendelea kutoa elimu ya msaada wa kisheria katika maeneo mbalimbali kama mirathi na ndoa.

Miongoni mwa wananchi walionufaika na msaada wa kisheria kutoka TANLAP, Elizaberth Mwaijande, alisema ni miaka tisa sasa tangu mumewe, Alex Mbetwa, afariki dunia na kumwachia watoto watatu, familia ya ndugu wa marehemu walimfukuza kwenye nyumba aliyokuwa akiishi.

Alisema uamuzi huo uliafikiwa na ndugu wa marehemu kwamba hana sababu ya kuendelea kuishi hapo na kuamua kumiliki mali zote za mumewe.

Alisema ndoa yake ilitambulika kwa mujibu wa sheria na kwamba aliamua kwenda mahakamani na kushinda kesi, lakini bado ndugu wa mumewe hawataki aishi kwenye nyumba ya mumewe.

"Mume wangu alipofariki nilifukuzwa kama mwizi nikiwa na watoto wangu watatu nilichofanikiwa kubeba ni nguo tu, nimeacha nyumba na mashamba ambayo ndugu wa muwe wanayatumia naumia kwa sababu hizo mali tulichuma na mume wangu... nahangaika kusomesha na kuhudumia peke yangu watoto, nimetishiwa kuuawa," alisema Mwaijande.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kikota, Asubisye Gwambusisya, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyoikabili eneo lake ni migogoro ya ardhi na mirathi.

Alisema mara kwa mara amekuwa akipokea malalamiko kuhusu suala la watu kugombania mipaka na wakati mwingine kutishiana maisha.

Alidai kuwa awali alikuwa hajui namna bora ya kushughulika na matatizo hayo, na kwamba elimu ya msaada wa kisheria waliyoipata kutoka TANLAP itamsaidia kutatua matatizo hayo.




Mkurugenzi wa Sauti ya Haki Tanzania, Wakili Laetitia Petro, jana, akitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi wa Kijiji cha Kikota wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa Mwanamke Imara unaotekeleza na Taasisi ya Tanzania Network of Legal Aid Providers. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Chunya yapata matumini ya barabara

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI imepanga kujenga kilomita 58 za barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na mikoa ya Tabora na Singida kuanzia katika Mji wa Makongolosi wilayani Chunya kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Hayo yalisemwa juzi na Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alipokuwa anazungumza na wananchi wa Mji wa Makongolosi kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo.

Alisema kwa sasa barabara ya Chunya- Makongolosi yenye urefu wa Kilomita 39 umekamilika, hivyo katika bajeti iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni zimetengwa fedha kwa ajili ya kuendeleza barabara hiyo, na kwamba barabara hiyo itakuwa inajengwa kwa awamu tofauti.

Alisema mbali na barabara hiyo, pia zipo barabara mbalimbali ambazo zitaboreshwa na serikali ili kuwasaidia wananchi wa maeneo ya pembezoni mwa miji kusafiri na kusafirisha mazao yao bila vikwazo vya aina yoyote.

"Serikali imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya uboreshaji wa barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika wilaya yetu hivyo naamini kuwa barabara nyingi zitaboreshwa," alisema Kasaka.

Vilevile, alisema katika wilaya hiyo kuna vijiji 12 na vitongoji 14 ambavyo mpaka sasa havijafikiwa na umeme, lakini akadai kuwa tayari makandarasi wanaendelea na kazi ya kusambaza nishati hiyo kwenye vijiji vyote.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha vijiji vyote nchini vinaunganishiwa nishati hiyo ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao ikiwamo uanzishwaji wa viwanda vidogo.

# Mil. 500/- sasa kujenga barabara Chimala-Kapunga

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

KATIKA kuhakikisha wananchi wananufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo, serikali wilayani Mbeya imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chimala-Kapunga yenye urefu wa Kilomita 26.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema eneo la Kapunga ni miongoni mwa maeneo wilayani humo yenye wawekezaji wakubwa yakiwapo mashamba makubwa ya Kapunga Estate pamoja na wakulima wadogo, hivyo barabara hiyo ni muhimu.

"Kwa muda mrefu wananchi walikuwa wanaahidiwa kwamba barabara hii itaboreshwa, sasa tumeshapokea fedha hizi na tumeshatoa maelekezo kwa maofisa wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili waanze kuijenga," alisema Mfune.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali ikiwamo kulinda vifaa vitakavyotumika kwenye ujenzi wa mradi huo ili visiibiwe pamoja na kukubali kupisha mradi huo kwa wale ambao watalazimika kuhamishwa.

Vilevile, alisema halmashauri hiyo imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya inayojengwa katika eneo la Rujewa ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Kadhalika, alisema wanaendelea kushirikiana na wananchi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa 127, ili kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaotarajia kuanza masomo mwezi Januari mwakani.

**"Kwa muda mrefu wananchi walikuwa wanaahidiwa kwamba barabara hii itaboreshwa, sasa tumeshapokea fedha hizi na tumeshatoa maelekezo"**



## Washauriwa kuchangamkia fursa za UN

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZANZIBARI wametakiwakuchangamkia fursa zinazotolewa na Umoja wa Mataifa ili kufaidika nazo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa elimu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu Zanzibar kuhusu kuchangamkia fursa zinazotolewa na UN kupitia mpango wa kujitolea, mtaalamu wa dibwi la vipaji wa UN, Penina Nguma, alisema bado ushiriki wa Wazanzibari ni mdogo katika kuchangamkia fursa zinazotolewa na umoja huo katika kujitolea.

Penina alisema wameamua kutoa elimu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu Zanzibar, ili wanapomaliza masomo yao kuchangamkia fursa zinazotolewa na UN na kwamba zitawasaidia kupata kipato kidogo na kujijenga kiuwezo.

Alisema UN kupitia mpango wa kujitolea, ipo katika mchakato wa kutafuta vijana wa kizanzibari wenye sifa na vigezo vitakavyowawezesha kuingia katika programu za kujitolea ndani na nje ya Zanzibar.

Alieleza kuwa vijana wengi wanaposikia suala la kujitolea huwa wagumu huona kuwa wanajitolea bure, lakini wanapojitolea hupata fursa nyingi zenye faida.

"Kwa sasa Zanzibar tumeshatoa elimu kwa vijana wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZDU), lakini tunatarajia kuendelea kutoa elimu kwa vyuo vingine," alisema.

Naye Rais wa Serikali ya wanafunzi wa SUZA, Suleyum Abdallah Ali, alisema elimu waliyopatiwa na UN itasaidia kuchangamkia fursa zinazotolewa, kwa sababu ushiriki wa vijana wa kizanzibari ulikuwa mdogo kutokana na hawakuwa na uelewa.

"Mafunzo ni mazuri sana kwa sababu unaposikia kujitolea huona kuwa hakuna faida unayoipata, kumbe kujitolea katika shirika hili la kimataifa kutakujengea mazingira mazuri katika kupata ajira," alisema.

Aliwaasa wanafunzi waliomaliza chuo wasikae nyumbani, badala yake kuitumikia jamii kwa kujitolea ambapo kujitolea kutawasaidia kuwajengea mazingira mazuri ya kupata ajira.

Mwakilishi mkazi wa umoja huo, Christian Mwamanga, alisema mchakato huo unatafuta vijana wa kada tofauti ikiwamo mtaalamu bingwa wa mataifa wa kujitolea na kijana wa UN kwa njia ya mtandao.

# Rais Mwinyi aeleza sababu za utumbuaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hatua anazozichukua za kuwatumbua watendaji zinalengo la kuimarisha utendaji serikalini na sio kumwonea mtu.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akiwahutubia wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi baada ya kulizindua Tawi la CCM la Sebleni lililojengwa upya pamoja na kuzindua kisima cha majisafi na salama Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema maamuzi anayoyafanya si kwa nia mbaya bali ni kwa nia njema ili kuhakikisha mapato yanaingia serikalini.

"Ninachokifanya ni kwa ajili ya kusaidia wananchi na kuhakikisha utendaji serikalini unakuwa bora zaidi na watu wanapata huduma bora baada ya kuruhusu watu wachache kuchukua fedha hizo kwa maslahi yao binafsi," alisema.

Dk. Mwinyi aliongeza: "Najua hatua zile zitaleta taharuki kwa watu wachache, lakini niwahakikishie tunachukua kwa nia njema na pale inapothibitika kuna mtendaji ambaye amesimamishwa kazi bila ya makosa, watarudishwa katika utumishi wa umma."

Rais Dk. Mwinyi alieleza mpango ya serikali anayoiongoza ya ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 220 katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba ambao utafanyika ndani ya miezi 24.

Alisema kwa upande wa sekta ya afya mipango madhubuti imeshapangwa katika kuhakikisha serikali inaiimarisha sekta hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza huduma, kazi ambayo itadharimu Dola milioni 100, zilizotolewa kwa ajili ya mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Aidha, alisema kuwa uongozi wa Jimbo la Kwahani umetekeleza mambo makubwa mawili likiwamo la kuimarisha CCM pamoja na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wa jimbo lao hilo, hatua ambayo ameipongeza.

Alisema kuwa viongozi wa jimbo hilo wameshafanya kazi nyingi katika kutoa huduma za jamii ikiwamo ujenzi wa kisima cha majisafi na salama kazi ambazo zimefanywa kwa ushirikiano.

Viongozi wa jimbo hilo walieleza kwamba wanaridhika na uongozi wa Rais Dk. Mwinyi ambao umeweza kuendeleza amani, umoja, utulivu na mshikamano.

Mbunge wa Jimbo hilo, Yahya Idrisa Abdulwakil, aliwataka wananchi na wanachama wa CCM waweke matarajio makubwa na mambo mazuri zaidi yanakuja, huku wakisisitiza kwamba mafanikio ya jimbo lao yanatokana na umoja na ushirikiano na kukiimarisha (CCM). Naye Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Mjini Kichama, Tali Ali Talib, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kutokana na juhudi zake za uongozi pamoja na kuwapongeza viongozi wa jimbo hilo kwa ushirikiano katika kuwaletea maendeleo wananchi.



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) wakiwa pamoja na mkufunzi wao, Penina Nguma (wanne kulia), baada ya kupewa elimu ya kujitolea katika Shirika la Umoja wa Mataifa kupitia mpango wa kujitolea. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tumbatu yalalamikia kukosekana watendaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKAZI wa Kisiwa cha Tumbatu Zanzibar wamesema kukosekana kwa watendaji katika ofisi ya wilaya ndogo kisiwani humo ni kikwazo kikubwa kwao.

Waliyasema hayo juzi mbele ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, alipofika katika kisiwa hicho wakati wakiwasilisha changamoto zao kwa kiongozi huyo.

Jabu Khamis, alisema hali hiyo inawalazimu kusafiri kwenda kufuata huduma muhimu ikiwamo vyeti vya kuzaliwa katika maeneo ya mbali.

Aidha, alisema kitendo cha kufuata huduma katika maeneo ya mbali kinasababisha kuingia katika gharama zaidi pamoja na kupoteza muda.

Asha Juma, alisema wanakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa wataalamu wa afya pamoja na vifaa muhimu kwa ajili ya huduma za kinamama wanaotaka kujifungua.

"Kituo cha afya tunacho, lakini tatizo kubwa ni wataalamu wa afya pamoja na vifaa tiba hasa kwa huduma za mama na mtoto," alisema.

Aidha, aliiomba serikali kuwaboreshea huduma muhimu kijijini hapo hasa ikizikangatiwa kuwa jiografia ya kisiwa cha Tumbatu kimezungukwa na bahari, hivyo huwalazimu kutumia usafiri wa baharini kufuata huduma maeneo mengine.

Naye Abdullah alisema serikali imeweka kipaumbele katika kuimarisha huduma za kijamii, lengo likiwa ni kutatua vikwazo vinavyowakabili wananchi wake.

Alieleza kuwa kuwapo kwa umoja na ushikamano kutatoa fursa kwa serikali kuimarisha huduma bora ambazo zitawalenga wananchi wote bila kujali tofauti walizonazo.

Aidha, aliwataka wananchi na wakazi wa Tumbatu kukaa pamoja ili kuzipatia suluhu tofauti ndogo zilizomo ndani ya jamii kwa lengo la kumsaidia Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kuleta maendeleo.

Aliwaagiza mawaziri na viongozi alioambatana nao kukaa na kuja na mpango maalum wa kutatua kero za wananchi.

Alieleza kuwa serikali ya awamu ya nane itaweka historia kwa kuhakikisha Tumbatu inakuwa na miundombinu ya barabara zitakazojengwa kwa kiwango cha lami.

Pia alisema serikali imepanga kukuza uchumi wa nchi kupitia uchumi wa bluu na kuanzisha viwanda, jambo ambalo litasaidia wananchi wengi kujiajiri na kuwarahisishia upatikanaji wa huduma na bidhaa tofauti nchini na kuacha kuagiza nchi zingine.

Wakijibu changamoto zilizowasilishwa na wakaazi wa Wilaya ndogo ya Tumbatu, viongozi wa taasisi mbalimbali pamoja na mawaziri walimwakikishia Makamu wa Pili wa Rais kuwa changamoto hizo watazipatia ufumbuzi ndani ya muda mfupi.

# Chongolo awaonya wana CCM wanapowachagua viongozi

**Na Beatrice Shayo,** MASASI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka wanachama kutafuta viongozi wenye sifa ya kukitumikia chama vizuri na siyo wafuasi kwa kuwa kwa kufanya hivyo watawaumiza wananchi.

Chongolo aliyasema hayo juzi wakati wa majumuisho ya ziara ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara.

Alisema kumekuwa na majungu mengi yanayoendelea ndani ya chama ya watu wanaoandaliwa kutafuta viongozi, jambo ambalo linakiharibia chama kwa kuwa linajenga makundi.

Aidha, Chongolo alisema kwa sasa uendeshaji wa shughuli za serikali umeonekana kufanya vizuri na kwamba tatizo lipo kwa watendaji ndani ya chama.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, watendaji wa chama wamekuwa wakivutana mashati jambo ambalo linawasababishia watumishi wa serikali kushindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na hali hiyo.

"Kuna changamoto katika uhusiano upande wa serikali, yapo vizuri kwenye chama, wanavutana mashati acheni majungu acheni majungu," alisisitiza Chongolo.

"Tuogope watu wanaoandaliwa na watu kuwa viongozi hii ni hatari kutengeneza viongozi wananchi msikibali tunajitafutia matatizo na hata kukosa maendeleo," alisisitiza.

Aidha, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh.

bilioni 60 kwa ajili ya pembejeo mwanzo wa msimu, kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kupata faida kubwa na hakuna mkulima atakayekatwa fedha hizo kama ilivyokuwa awali.

Alisema mwaka huu, Rais Samia ameelekeza korosho zote kupakiwa katika Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kusafirishwa na siyo Dar es Salaam kama ilivyokuwa awali.

Chongolo alisema bandari hiyo imegharimu zaidi ya Sh. bilioni 100 kwa ajili ya upanuzi, ili kuiongozea uwezo na kuwanufaisha wananchi pamoja na taifa katika kupata mapato.

Katibu Mkuu huyo alisema CCM inaridhishwa na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kama ujenzi wa uwanja mpya wa ndege Mtwara.

Aidha, alimpongeza Katibu wa Halmashauri ya Taifa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, kwa kutatua mgogoro uliodumu kwa miaka 10 baina ya wananchi na mamlaka ya uwanja huo.

Chongolo aliwaagiza viongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kutoka ofisini na kushirikiana na taasisi nyingine kupima ardhi ili kumaliza migogoro inayojitokeza.

Kuhusu malalamiko ya wananchi, alisema maeneo mengi waliyotembelea kilio kikubwa ni ukosefu wa majisafi na salama pamoja na umeme, na kuzitaka wizara hizo kushughulikia tatizo hilo kwa haraka.



Meneja mauzo wa kampuni ya GF TRUCKS & Equipment's Ltd, Paul Msuku (kulia), akizungumza na wateja waliotembelea banda lao wakati wa maonyesho ya madini mkoani Geita jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atilia shaka maamuzi ya wanasiasa waliopita

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imesema maamuzi ya wanasiasa nchini yalichangia kuua mashirika ya umma na kwamba kwa sasa haiwezi kurudia makosa kama hayo.

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokagua ujenzi wa kiwanda cha kukoboa mpunga kinachoko jijini Mwanza.

Kiwanda hicho kinajengwa na serikali kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, ili kusaidia upatikanaji wa mchele wenye ubora ambao utauzwa ndani na nje ya nchi.

Alisema mashirika mengi ya umma likiwamo Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) yalikufa kutokana na wanasiasa kuingilia utendaji na maamuzi ya uongozi uliokabidhiwa kufanya kusimamia.

"Hapa tunatarajia kiwanda hiki kijiendeshe kwa faida na kugawa pato lake kwa serikali hatutarajii hasara hata siku moja hapa," alibainisha Profesa Mkenda.

Kwa mujibu wa waziri huyo, uongozi wa kiwanda hicho utakuwa na maamuzi yake yanayojitegemea na kwamba hakuna mwanasiasa atakayewaingilia katika shughuli zao za kila siku.

"Hawa watapanga mipango yao wenyewe, watatafuta malighafi wenyewe, watakoboa na kuuza wenyewe, serikali inataka kuona faida imepatikana," alifafanua.

Prof. Mkenda alisema kiwanda hicho kitakuwa kinanunua zao la mpunga kutoka kwa wakulima na kukoboa kisha kuuza nje ya nchi na kwamba kwa sasa soko ni kubwa katika nchi mbalimbali.

Alitaja nchi ambazo zinazohitaji mchele wa Tanzania ni pamoja na Sudan Kusini, Afrika Kusini, Zimbabwe, Kenya, Nigeria na kwamba ujenzi huo utagharimu Sh. bilioni 6.68 mpaka kukamilika kwake.

Aidha, alisema kiwanda hicho kitakapokamilika kitatoa ajira kwa watu 26 hadi 30 wa moja kwa moja na kwamba wengine watafaidika kwa njia ambazo siyo za moja kwa moja.

Profesa Mkenda alisema serikali imewekeza teknolojia ya kisasa katika kiwanda hicho na kwamba kitakuwa na uwezo wa kukoboa tani tano kwa saa moja.

Waziri huyo alisema asilimia 80 ya malipo ya mradi huo yameishatolewa na kwamba kitaanza kufanya kazi Oktoba 18, mwaka huu.

Naye Meneja wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyika Kanda ya Ziwa, Stephene Kubena alisema licha ya kununua mpunga, watawasaidia wakulima kulima kilimo chenye tija.

Alisema watawafuatilia wakulima hao ili kuhakikisha wametumia mbegu bora ambayo itashindana sokoni.

Aidha, alisema watakapoanza kununua mpunga hakutakuwa na madalali ama mtu wa kati na kwamba mkulima atafika kiwandani hapo na kuuza mali yake mwenyewe na kupewa malipo.

Kubena aliwataka wakulima kutoka mikoa mbalimbali ya nchi kuchangamkia fursa hiyo na kwamba watakuwa wanatoa bei nzuri ili kuwanufaisha wakulima.

# Mradi mkubwa kuleta neema ya maji Moro

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO.

WIZARA ya Maji kwa kushirikisha taasisi, viongozi wa serikali na wadau muhimu, imeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuboresha upatikanaji wa huduma za maji Manispaa ya Morogoro.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya kusainiwa mkataba na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) wenye thamani ya Euro milioni 70.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, alisema hayo wakati akifungua kikao cha wataalamu na wadau kuanza kazi ya kutafuta na kuandaa mpango wa vyanzo vipya vya maji.

Alisema Mei 27, 2019 serikali ilitia saini mkataba na AFD wenye thamani ya Euro milioni 70 ili kutekeleza mradi huo wa kuboresha huduma za maji katika Manispaa ya Morogoro.

Mhandisi Kemikimba alisema, kiasi hicho ni takribani Sh. bilioni 185 kati ya hizo, Sh. bilioni 154 ni mkopo wa masharti nafuu kutoka AFD na takribani Sh. bilioni 31 ni mchango wa serikali.

Alitaja baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na mradi huo pamoja na kazi za matokeo ya haraka, ni ujenzi wa mtambo mpya wa kisasa wa kusafisha maji utakaozalisha maji kiasi cha lita milioni 54 kwa siku.

Alisema lengo ni kuongeza nguvu mtambo uliopo wa Mafiga unaozalisha lita milioni 27 kwa siku, hivyo kufanya uzalishaji kufikia kiasi cha lita milioni 89 kwa siku ifikapo mwaka 2025 ikilinganisha na mahitaji ambayo ni lita milioni 67 kwa siku.

Kazi nyingine ni kuboresha Bwawa la Mindu, kujenga bomba lenye ukubwa wa kipenyo cha milimita 700 (Inch 28) kutoka Bwawa la Mindu kwenda kwenye mtambo wa kutibu maji wa Mafiga ili kuongeza uzalishaji na ujenzi wa matangi yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 12.

Pia ujenzi wa mtandao wa kusambazia maji kilometa 75 kwa maeneo ya Kata ya Mkundi, Lukobe na Kingolwira, kupanua mtandao wa majitaka, ukarabati wa mabwawa ya kutibu majitaka Mafisa na kufanya kampeni za kuwajengea uelewa wananchi kwa kutoa elimu juu ya usafi wa mazingira.

Alitaja kazi nyingine ni kutafuta vyanzo vipya vya maji katika wilaya ya Morogoro vitakavyotosheleza mahitaji ya maji hadi kufikia mwaka 2040.

"Leo tupo hapa ikiwa ni kikao cha kwanza (Kickoff - Meeting), cha kuanza kazi ya kutafuta vyanzo vipya vya maji ili kukudhi mahitaji ya sasa hadi mwaka 2040 katika Manispaa ya Morogoro," alisema Mhandisi Kemikimba.

Alisema kuwa, Mtaalamu Mshauri Arteria toka Ufaransa kwa kushirikiana na Norplan wa Tanzania amepewa jukumu hilo ikiwa na kufanya upembuzi yakinifu ili kuinua tuta la Bwawa la Mitu kwa mita 2.5.

Pia kufanya utafiti wa visima virefu na zabuni ya kupata makandarasi wa kuendeleza vyanzo vitakavyoainishwa ili kutatua changamoto ya maji katika Manispaa ya Morogoro.

Mhandisi Kemikimba alisema, ni matarajio ya serikali kuona mpango huo unakamilika kufikia Aprili, 2023 ambapo kazi hiyo itagharimu takribani Sh. bilioni 2.5 fedha za kitanzania.

## HABARI KIMATAIFA

**SHUJAA KIMBARI;**

# Rusesabagina kufungwa maisha leo?

**Kigali,** RWANDA

UAMUZI katika kesi ya Paul Rusesabagina umepangwa kutolewa leo.

Mpinzani huyo wa Paul Kagame, alifahamika kwa kuokoa watu zaidi ya 1,000 wakati wa mauaji ya kimbari ya Watutsi, anashtumiwa ugaidi tangu Februari mwaka jana. Katika kesi hiyo anaweza kukabiliwa na kifungo cha maisha.

Uamuzi katika kesi ya Paul Rusesabagina, anayeelezwa kuwa shujaa katika filamu ya mwaka 2004 ya Hollywood ya 'Hotel Rwanda' kuhusu mauaji ya kimbari, utatolewa leo, Septemba 20 baada ya kuahirishwa mara kadhaa.

Paul Rusesabagina anayejulikana kwa kuokoa maisha ya maelfu wakati wa mauaji ya kimbari ya Watutsi mnamo 1994, alion-doka nchini Rwanda kabla ya kuwa mpinzani na mkosoaji mkuu wa Rais Paul Kagame.

**Paul Rusesabagina, anakabiliwa na kifungo cha maisha na washtakiwa wenzake 20.**

Mwaka mmoja uliopita, alikamatwa na kutekwa nyara kulingana na familia yake, na kurudishwa Kigali ambako tangu wakati huo anakabiliwa na mashtaka ya ugaidi. Hukumu ilikuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu ambayo ilipangwa kutolewa Agosti 19, iliahirishwa hadi leo.

Hukumu ya kesi hiyo iliahirishwa kwa mwezi mmoja kwa sababu ya ukubwa wa kesi hiyo, mahakama ya Rwanda ilisema. Paul Rusesabagina, anakabiliwa na kifungo cha maisha na washtakiwa wenzake 20.

Wote wanashukiwa kuwa katika kundi la FLN, kundi lenye silaha ambalo lilidai kuhusika na mashambulio Kusini mwa Rwanda mwaka 2018.

Kundi hilo linachukuliwa kama tawi la kijeshi la MRCD, vuguvugu la upinzani la Paul Rusesabagina.

Tangu kuanza kwa kesi hiyo ya muda mrefu, familia ya Paul Rusesabagina inalaani kuingiliwa kwa mahakama na serikali na kutaka aachiliwe. Hivi karibuni Ubelgiji na Bunge la Ulaya, walielezea wasiwasi wao juu ya mazingira ya kukamatwa kwake na jinsi kesi hiyo inavyoshughulikiwa. Sio kesi ya haki, kulingana na Rusesabagina.

Paul Rusesabagina, alikanusha kuhusika kwake katika mashambulio yaliyoua watu kadhaa nchini Rwanda, kulingana na mamlaka.

Machi, mwaka huu alikataa kuripoti mahakamani, akidai kwamba hatapata haki katika kesi hiyo.

Kwa miezi kadhaa, mawakili wake wamehakikisha kwamba mamlaka ya Rwanda inazuia upande wa utetezi kumletea mteja wao nyaraka zinazohusu utaratibu wa kesi hiyo.

Hivi karibuni Rais Kagame alisema anataka kuona haki inatendeka katika kesi ya Rusesabagina. Katika mahojiano na France 24, rais alionya vitendo vya 'kibaguzi' dhidi ya mifumo ya kimahakama.

"Nataka kushuhudia mwenyewe haki katika kesi hiyo. Kwa nini unafikiria haki ni ya Ulaya au Marekani au kwa mwingine yeyote lakini sio sisi?" Alisema Rais Paul Kagame katika mahojiano na France 24. **RFI**



Mwigizaji maarufu wa filamu iitwayo 'Hotel Rwanda' Paul Rusesabagina (katikati) ambaye anatuhumiwa kwa mauaji ya kimbari, akizungumza na wakili wake, David Rugaza (kulia), kwenye Mahakama ya Nyarugenge mjini Kigali. Hatima ya kesi ya Rusesabagina kujulikana leo, nchini Rwanda. **PICHA: MAKTABA**

## Bouteflika azikwa na mashujaa wa uhuru

**Algiers,** ALGERIA

RAIS wa zamani wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika, aliyefariki dunia mwishoni mwa wiki, na amezikwa jana kwenye makaburi ya mashujaa ya El Alia huko Algiers, yaliyotengwa kwa mashujaa wa vita vya uhuru, ingawa hakuzikwa kwa heshima zote sawa na watangulizi wake.

Bouteflika (pichani), aliyeondolewa mamlakani mwaka 2019 baada ya kuitawala Algeria kwa miaka 20, alifariki dunia siku ya Ijumaa akiwa na umri wa miaka 84 katika nyumba yake, Zeralda, Magharibi mwa Algiers.



Alizikwa baada ya sala ya Dhuhur, kwa mujibu wa televisheni ya serikali.

Mwili wake ulipelekwa kwenye makao makuu ya Bunge, katikati mwa Algiers, viongozi mbalimbali serikalini na raia walitoa heshima za mwisho.

Watangulizi wake wote walizikwa, ikiwa ni pamoja na watu mashuhuri na mashahidi wa vita vya uhuru mwaka 1954 had 1962.

Algeria imetangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kuanzia juzi, kutokana na kifo cha rais wa zamani wa taifa hilo, Abdelaziz Bouteflika.

Ofisi ya rais huyo wa sasa ilisema katika maombolezo hayo ya siku 3 bendera zitapepea kwa nusu mlingoti. **RFI**

## Shule kwa wavulana, walimu wa kiume

**Kabul,** AFGHANISTAN

SHULE za sekondari zimefungua milango tena ingawa ni kwa ajili ya wavulana tu bila wasichana.

Watawala wapya wa nchi hiyo, Taliban, wameamuru wavulana na walimu wa kiume pekee, ndio warejee madarasani.

Walipoingia madarakani baada ya kuitimua serikali iliyoungwa mkono na Marekani mwezi uliopita, Taliban waliahidi kuachana na sera za mrengo mkali wa Kiislamu, kama ule walioushikilia miaka ya 1990.

Wakati huo kwa sehemu kubwa, wanawake na wasichana walitengwa katika vyuo vya elimu na kwenye nafasi za ajira.

Kabla ya kuanza upya kwa shughuli za masomo juzi, wizara ya elimu ilitoa tangazo, ambalo liliwataka 'walimu wote wa kiume na wanafunzi wavulana kupaswa kuripoti katika taasisi za elimu.

Tangazo hilo lililochapishwa juzi, halikusema chochote kuhusu walimu wanawake na wanafunzi wa kike.

Afghanistan, ni kawaida kuwatenganisha kwa msingi wa jinsia wanafunzi wa sekondari, ambao huwa ni kuanzia umri wa miaka 13 hadi 18.

Shule hizo zilikumbwa na vikwazo vya kufungwa mara kwa mara wakati wa janga la Covid-19 na tangu Taliban walipochukua hatamu ya uongozi, shule hizo zilikuwa zimefungwa kabisa. **DW**

## Wakosoaji wa Alpha Condé warejea Guinea

**Conakry,** GUINEA

VIONGOZI wakuu wanne wa upinzani na wakosoaji wakuu wa Alpha Condé, ambao waliitoroka nchi kuhofia usalama wao, wamerejea mwishoni mwa wiki, wakitokea uhamishoni.

Wapinzani hao wakubwa dhidi ya marekebisho ya katiba na kuwania kwa Alpha Condé kwa muhula wa tatu walikuwa wamekimbilia nje ya nchi.

Karibu wiki mbili baada ya mapinduzi, Ibrahima Diallo, Sékou Koundouno, mwanamuziki Djani Alfa na mwanablogu Fodé Sanikayi Kouyaté walilakiwa kama mashujaa na umati mkubwa wa watu, Conakry.

Wapinzani hao wameelezea furaha yao kuona wamerejea nchini mwao na kusema kuwa bado vita vinaendelea kuhakikisha demokrasia inakita miziza Guinea. **RFI**

MECHI KALI

HOME

AWAY

UDINESE

4.23 | 3.62 | 1.84


NAPOLI

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# ARTETA ASIFIA MORALI YA NYOTA ARSENAL

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alionyesha kufurahishwa kwake na morali ya upambanaji ya wachezaji wa Arsenal wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Burnley kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

'Washikabunduki' hao huo ulikuwa ni mchezo wao wa pili mfululizo kupata ushindi, wakati Martin Odegaard alipofunga kwa mkwaju wa adhabu ndogo kipindi cha kwanza pale kwenye Uwanja wa Turf Moor.

Burnley walikuwa wakali zaidi kipindi cha kwanza na walizawadiwa penalti baada ya golikipa Aaron Ramsdale kuonekana kumchezea vibaya Matej Vydra katika dakika ya 20.

Mwamuzi Anthony Taylor alibadilisha maamuzi ya penalti hiyo baada ya kujiridhisha na marudio ya VAR.

Arsenal walishinda mchezo huo wa pili mfululizo kwa mara ya kwanza tangu Desemba 2014 na kocha Arteta aliwasifia wachezaji wake kwa kuwa na ari kubwa kwenye mechi hiyo na pia wameimarika kiuchezaji.

Aliiambia BBC Sport: "Ulikuwa mchezo mgumu na hakika tulistahili ushindi na ndicho kilichotokea.

"Unatakiwa kuwa tayari kupambana wakati wote. Kipindi cha kwanza ni kama tulitawaliwa na tulipata nafasi ambazo hatukuweza kufunga mabao.



# *Varane: Kutua United ni ndoto iliyotimia*

**MANCHESTER,** England

PAPHAEL Varane anaamini anatimiza ndoto yake baada ya kujiunga na Manchester United kutoka Real Madrid.

Mlinzi huyo wa kati alishinda mataji matatu ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akicheza kule nchini Hispania, huku pia akishinda Kombe la Dunia mwaka 2018 akiwa na Ufaransa.

Varane, ambaye alijiunga na Madrid mwaka 2011 akitokea Lens, alikamilisha uhamisho wa kutua United uliokuwa na thamani ya pauni milioni 42.7 kipindi cha dirisha la majira ya joto lililopita.

Hata hivyo, katika mahojiano na Sky Sports, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amebainisha kwamba, alikaribia kutua hapo Old Trafford miaka 10 iliyopita wakati kocha wa zamani wa United, Sir Alex Ferguson aliposafiri kwenda Lille kutaka huduma ya nyota huyo aliyekuwa na umri wa miaka 18 wakati huo.

"Ulikuwa wakati maalumu katika maisha yangu kwa upande wangu mimi na familia yangu," alisema Varane.


## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA







# BARCELONA WAMTAKA STERLING KWA MKOPO

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wanawania kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling, kwa mujibu wa Sport.

Barca imewapoteza wachezaji wake muhimu kutokana na kukabiliwa na ukata wa kifedha kabla ya kuanza kwa msimu huu wa 2021-22.

Nyota wao, Lionel Messi ametimkia PSG ambako ametua kwa mkopo, wakati Antoine Griezmann akirudi Atletico Madrid kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja.

Barcelona sasa hawana mshambuliaji mkali kwenye kikosi chake, baada ya Sergio Aguero aliyetua hapo kwa uhamisho huru kukumbwa na majeraha ambayo yamemweka nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Na sasa miamba hao wa Catalunya wanafikiria kumsalili nyota huyo wa timu ya taifa ya England.

Miamba hao wa LaLiga wapo tayari kumhakikisha nafasi ya kucheza mara kwa mara Sterling ikiwa ni sehemu ya kutaka kuimarisha kikosi chao.



# Guardiola atoa sababu sare na Southampton

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anahisi Manchester City hawakuwa kwenye kiwango bora cha kutosha kuweza kuifunga Southampton katika mchezo uliomalizika kwa suluhu kwenye Ligi Kuu England juzi, Jumamosi katika Uwanja wa Etihad.

Bingwa huyo mtetezi alitengeneza nafasi moja tu ya kufunga kupitia kwa Phil Foden katika dakika ya 90 na kufanya kuwa na idadi ndogo zaidi ya nafasi walizotengeneza kwenye Ligi Kuu tangu Machi 2017.

Man City waliingia kwenye mchezo huo wakitoka kushinda mabao 6-3 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig katikati ya wiki.

Na kocha huyo wa City alikubali kwamba, timu yake haikuwa kwenye kiwango cha kutosha kuweza kupata pointi zote tatu katika mchezo huo. Aliiambia Sky Sports: "Tumetoka sare dhidi ya timu nzuri kwa hakika walilinda vizuri lango.

"Walikuwa na wachezaji wazuri katikati kama (Oriol) Romeu, mmoja wa viungo bora kwenye Ligi Kuu.

"Ulikuwa mchezo mgumu, hatukuwa kwenye kiwango bora na tulishindwa kucheza vizuri na kwa hakika walitubana katika kila idara."

Guardiola aliongeza: "Kila mchezo ni tofauti kabisa. Tofauti na tulivyocheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huu ulikuwa ni mchezo mgumu sana."


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 20 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1895 | Alashkert Martuni vs FC Noravank | 1.38 | 4.46 | 6.97 |
| 15:00 | 3904 | Shukura vs Dinamo Tbilisi | 6.78 | 4.16 | 1.41 |
| 15:00 | 4208 | Sunderland U23 vs Middlesbrough U23 | 2.61 | 3.53 | 2.33 |
| 15:00 | 5336 | FC Samtredia vs Torpedo Kutaisi | 2.47 | 3.10 | 2.72 |
| 16:00 | 3724 | Universitatea Cluj vs ACS Sirineasa | 1.76 | 3.54 | 4.07 |
| 16:00 | 4743 | Swansea U23 vs Crewe U23 | 1.76 | 3.90 | 4.20 |
| 16:30 | 1879 | Ural Yekaterinburg vs Lokomotiv Moscow | 4.24 | 3.50 | 1.81 |
| 17:00 | 1914 | Boluspor vs Istanbulspor | 2.80 | 3.29 | 2.30 |
| 17:00 | 4101 | FK Turon vs Navbahor Namangan | 3.44 | 2.81 | 2.23 |
| 18:00 | 2455 | CSA Steaua Bucuresti vs ACS Viitorul Selimbar | 1.62 | 3.59 | 5.04 |
| 18:00 | 2464 | FC Telavi vs Dinamo Batumi | 12.61 | 5.43 | 1.20 |
| 18:00 | 3145 | Kvik Halden vs Valerenga IF 2 | 1.50 | 4.54 | 4.83 |
| 18:00 | 4585 | Dila Gori vs Saburtalo Tbilisi | 1.95 | 3.20 | 3.73 |
| 18:00 | 4678 | Kjelsaas vs Rosenborg BK 2 | 1.18 | 6.61 | 10.69 |
| 18:30 | 2919 | Rubin Kazan vs Zenit St Petersburg | 4.75 | 3.96 | 1.63 |
| 19:00 | 3362 | Omonia Nicosia vs Doxa Katokopia | 1.29 | 5.34 | 9.50 |
| 19:00 | 3406 | FCI Levadia Tallinn U21 vs FC Elva | 1.62 | 4.56 | 4.26 |
| 19:00 | 4326 | Skra Czestochowa vs Arka Gdynia | 5.04 | 3.59 | 1.62 |
| 19:30 | 5760 | CSKA Moscow vs Spartak Moscow | 2.45 | 3.35 | 2.71 |
| 20:00 | 1019 | IFK Varnamo vs Orgryte IS | 1.86 | 3.34 | 4.49 |
| 20:00 | 1228 | Academica vs Vilafranquense | 1.58 | 3.61 | 5.67 |
| 20:00 | 2008 | Qizilqum vs Otmk Olmaliq | 2.95 | 2.95 | 2.39 |
| 20:00 | 2049 | Wehen vs Borussia Dortmund II | 2.46 | 3.45 | 2.61 |
| 20:00 | 2821 | Ankaragucu vs Menemen Bld | 1.39 | 4.45 | 6.58 |
| 20:00 | 2958 | Silkeborg vs Aarhus | 2.26 | 3.55 | 2.86 |
| 20:00 | 2995 | Loko Tbilisi vs FC Samgurali Tskaltubo | 1.66 | 3.63 | 4.65 |
| 20:00 | 3048 | Hammarby vs Varbergs Bois | 1.58 | 3.96 | 4.73 |
| 20:00 | 4315 | Balikesirspor vs Keciorengucu | 4.16 | 3.34 | 1.80 |
| 20:00 | 5469 | AIK Football vs IFK Goteborg | 1.83 | 3.25 | 4.17 |
| 20:00 | 5501 | FC Trollhattan vs Utsiktens BK | 2.22 | 3.34 | 2.90 |
| 21:00 | 2332 | Newcastle U23 vs Stoke City U23 | 2.16 | 3.62 | 2.80 |
| 21:00 | 2641 | Jong PSV vs ADO Den Haag | 2.50 | 3.60 | 2.60 |
| 21:00 | 2781 | CFR Cluj vs Universitatea Craiova | 1.83 | 3.32 | 4.30 |
| 21:00 | 3631 | Wolverhampton U23 vs Fulham U23 | 1.97 | 3.77 | 3.10 |
| 21:00 | 4061 | Benfica vs Boavista | 1.19 | 6.31 | 12.81 |
| 21:00 | 4450 | Derby County U23 vs West Ham U23 | 3.39 | 3.82 | 1.86 |
| 21:00 | 4557 | Reading U23 vs Norwich U23 | 2.17 | 3.53 | 2.85 |
| 21:00 | 5285 | Nottingham U23 vs Birmingham U23 | 3.05 | 3.73 | 2.00 |
| 21:30 | 2826 | Leixoes vs Viseu | 1.65 | 3.72 | 4.80 |
| 21:30 | 4228 | Frosinone vs Brescia | 2.24 | 3.06 | 3.31 |
| 21:30 | 5966 | KS Gornik Polkowice vs GKS Katowice | 2.09 | 3.30 | 3.20 |
| 21:45 | 4770 | Udinese vs Napoli | 4.23 | 3.62 | 1.84 |
| 21:45 | 5629 | Bohemians FC vs Derry City | 1.69 | 3.58 | 4.45 |
| 22:00 | 1235 | Burgos vs Las Palmas UD | 2.51 | 2.95 | 2.95 |
| 22:00 | 4396 | Monopoli vs Avellino | 2.50 | 3.05 | 3.00 |
| 22:00 | 4712 | Concarneau vs Avranches | 2.01 | 3.15 | 4.10 |
| 22:00 | 5315 | Deportivo Santani vs General Caballero | 2.03 | 3.20 | 3.45 |
| 22:00 | 5718 | Barcelona vs Granada | 1.34 | 5.34 | 8.29 |
| 22:15 | 1678 | HK Kopavogs vs Stjarnan | 1.98 | 3.59 | 3.21 |
| 23:15 | 4564 | Sporting Braga vs Tondela | 1.33 | 5.12 | 7.87 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MANE AFIKISHA MABAO 100 KUIFUNGIA LIVERPOOL

Pia aweka rekodi ya kipekee kwa kuitungua zaidi Crystal Palace kwenye Ligi Kuu huku...

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imebakia kuwa timu ambayo haijapoteza mchezo kwenye Ligi Kuu England msimu huu, baada ya Sadio Mane kufunga bao lake la 100 kwa klabu hiyo katika ushindi dhidi ya Crystal Palace.

**Kikosi hicho cha kocha Jurgen Klopp kilitengeneza nafasi kadhaa dhidi ya Palace walionekana kuwa bora zaidi kipindi kwanza, kabla ya Mane kufunga bao la kwanza kipindi cha kwanza.**

Mohamed Salah alifunga la pili zikiwa zimesalia dakika 10 mchezo kumaliza kwa shuti kali, kabla ya Naby Keita kufunga la tatu dakika ya mwisho na kuifanya timu hiyo kuondoka na ushindi wa mabao 3-0.

Liverpool walipoteza nafasi nyingi kipindi cha kwanza, wakati shuti la Diogo Jota lilipaa juu ya goli akiwa peke yake, huku Thiago na Jordan Henderson mipira yao iliokolewa kwa ustadi mkubwa na golikipa, Vicente Guaita.

Palace walianza mchezo huo kwa kasi - wakikosa nafasi mbili za wazi za kufunga wakati Liverpool waliposhindwa kuokoa hatari langoni mwao.

Lakini mwisho wa siku ulikuwa ushindi mtamu kwa Liverpool pale Anfield, wakitoka kushinda mabao 3-2 dhidi ya AC Milan kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Hiyo inamaanisha kwamba, wapo kileleni mwa msimamo wakiwa wameshinda mechi zao nne kati ya tano, huku Palace wakibakiwa kuwa nje ya 10 bora.

Mane alikuwa mmoja kati ya mabadiliko sita aliyofanya Klopp kutoka kwenye kikosi kilichoifunga AC Milan, na kurudi kwake kulikuwa na maana zaidi kwake.

Akiwa alifunga mara mbili dhidi ya msimu uliopita, bao la ufunguzi la Mane lilimfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mara tisa mfululizo mechi za ligi dhidi ya mpinzani mmoja.

Mane sasa amefikisha mabao 13 aliyowafunga Palace kwenye Ligi Kuu akiwa ndio mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi dhidi ya timu hiyo na alifikisha bao lake la 100 kwenye mashindano yote kwa Liverpool.

## ZISIKUPITE

### UTD BADO WAMTAKA HALAAND

MANCHESTER United bado wanataka kumsajili straika wa Borussia Dortmund raia wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, licha ya kurudi kwa Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36. ***(Express)***

### MESSI MSHAHARA JUU PSG

LIONEL Messi ataingiza kiasi cha pauni milioni 25.6 kila msimu kwa misimu miwili ijayo pale Paris St-Germain, huku mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 34, mshahara wake sasa utaongezeka kwa pauni milioni 8.5 kama atabaki kwa mwaka mmoja zaidi. ***(L'Equipe, via Marca)***

### DE LIGT KUONDOKA JUVE

WAKALA wa Matthijs de Ligt, Mino Raiola amesema mlinzi huyo wa kati wa Uholanzi anaweza kuondoka Juventus mwishoni mwa msimu huu, huku Chelsea ikionyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Tuttosport, via Express)***

### ARSENAL YAONYWA KWA NEVES

KOCHA wa Wolverhampton Wanderers, Bruno Lage amezionya Manchester United na Arsenal kwamba hatamwachia kiungo wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 24. ***(Express)***

### RICE AWEKEWA NGUMU

KOCHA wa West Ham United, Kevin Nolan, amesema anaweza asimuuze kiungo wa England mwenye umri wa miaka 22, Declan Rice ambaye amekuwa akiwaniwa zaidi na Manchester United huku ada yake ikitajwa kuwa pauni milioni 100. ***(Manchester Evening News)***

### CAVANI HAONDOKI UNITED

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Edinson Cavani, hataki kuondoka Old Trafford licha ya straika huyo mwenye umri wa miaka 34 raia wa Uruguay, kukabiliwa na changamoto ya kugombea namba na Cristiano Ronaldo. ***(ESPN Brazil)***

### CHELSEA KWA TCHOUAMENI

CHELSEA inajiandaa kutoa ofa nzuri zaidi, ili kumsajili kiungo wa Monaco, Aurelien Tchouameni kutua Stamford Bridge huku pia Juventus wakiwa wamejitosa kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ufaransa. ***(Tuttomercatoweb, via Express)***

### DE GEA, HENDERSON VITANI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amekiri hajafanya maamuzi ya golikipa gani namba moja kwenye kikosi hicho msimu huu, huku Dean Henderson mwenye umri wa miaka 24 na David de Gea mwenye miaka 30, wakipambana kuwania nafasi hiyo. ***(Mirror)***

### CASH KUICHEZEA POLAND

MLINZI wa Aston Villa, Matty Cash ataombwa kuichezea Poland kabla ya kuanza kwa michuano ya kufuzu Kombe la Dunia, kwa sababu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anafuzu kuichezea nchi hiyo kwa sababu mama yake ni raia wa huko. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

## Odhiambo kumulika mabeki Biashara United

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo, amesema ana kazi kubwa ya kufanya hasa katika safu ya ulinzi na ushambuliaji kuelekea hatua ya kwanza ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Odhiambo alisema mbali na kupata ushindi wa mechi zote mbili nyumbani na ugenini bado ana kazi kubwa ya kufanya kuboresha kikosi chake kwenye nafasi ya ulinzi na ushambuliaji.

"Kwenye mechi hizi mbili tulizocheza kuna mapungufu yamejitokeza ukiangalia zaidi ni safu ya ulinzi maana mara kadhaa FC Dikhil wamekuwa wakifika katika eneo letu, pia washambuliaji wetu wamekosa nafasi nyingi za wazi," alisema Odhiambo.

Aidha, Odhiambo alieleza kufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo wao wa wa raundi ya pili dhidi ya timu ya FC Dikhil.

"Ninashukuru kwa matokeo tuliyoyapata tunaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano tuweze kutimiza malengo tuliyojiwekea,"alisema.

## Tanzanite Queens yamkuna Jokate

**Na Shufaa Lyimo**

MKUU wa Wilaya ya Temeke Jokate Mwegelo ameipongeza timu ya Taifa ya Wanawake wenye umri chini ya miaka 20, Tanzanite Queens kwa kufanikiwa kubeba Kombe la Tanzanite katika Tamasha la Michezo la Wanawake la Tanzanite, lililozinduliwa juzi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Katika tamasha hilo lililozinduliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenista Mhagama kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan Tanzanite Queens ilibeba kombe hilo kwa kuifunga Simba Queens kwa penalti 2-1 baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Jokate alieleza kufurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wanawake katika tamasha hilo ambalo lilikuwa na mvuto wa aina yake.

"Ninaipongeza timu ya Tanzanite kwa kufanikiwa kupata kombe kwenye Tamasha la Wanawake la Tanzanite, nimefurahi nimeona michezo mbalimbali," alisema Jokate.

Aidha, Jokate alisema Temeke ni wilaya pekee ambayo imeibua vipaji mbalimbali vya wachezaji na kuahidi kuviendeleza.

# AZAM YAGEUKIA LIGI KUU, YAIPOTEZEA PYRAMIDS CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuvuka raundi ya awali kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, benchi la ufundi la Azam FC, limesema akili na mipango yao kwa sasa wanaihamishia kusaka pointi tisa za mechi tatu za msimu mpya wa 2021/22 wa Ligi Kuu Tanzania.

Azam ambayo juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Horseed SC ya Somalia hivyo kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa jumla ya mabao 4-1, sasa inasubiri kuwakaribisha matajiri wa Misri, Pyramids katika mechi ya mkondo wa kwanza itakayochezwa Oktoba 15, mwaka huu kabla ya kwenda kurudiana ugenini siku saba baadaye.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema baada ya kuvuka hatua ya mkondo wa kwanza, akili na nguvu zao sasa ni kwenye mechi tatu za ligi kabla ya kukutana na Pyramids michuano hiyo ya CAF.**

Alisema kwa sasa wanaangalia mechi tatu wakianza dhidi ya Coastal Union mchezo utakaochezwa Septemba 27, mwaka huu na baada ya hapo wataenda Kilimanjaro kuwavaa Polisi Tanzania na kisha kurudi Dar es Salaam kumalizina na Yanga.

"Tunahitaji kufanya vizuri msimu huu wa ligi, tupambane kupata pointi zote tisa na baada ya mechi hizo, tutakuwa tumeimarika zaidi na kuanza kufikiri mchezo wetu wa kimataifa dhidi ya Pyramids," alisema Bahati.

Alisema msimu huu malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi katika Ligi Kuu kwa kuvuna pointi muhimu katika kila mechi pamoja na kufanya vizuri michuano ya kimataifa kwa kusonga mbele hadi kucheza hatua ya makundi.

"Mechi za ligi zitatusaidia kuimarika na kuwa bora zaidi kukutana na wapinzani wetu Pyramids, timu yenye uzoefu mkubwa wa michuano hii ya kimataifa na tunahitaji kufanya vizuri kufikia malengo yetu," alisema kocha huyo.




Beki wa Kati wa Simba, Pascal Wawa, akicheza na Mascot wa klabu hiyo wakati wa utambulisho wa wachezaji wa timu hiyo kwenye Tamasha la Simba Day lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *10 bet yatua Afrika, yaitoa Dodoma Jiji FC*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kimataifa ya mchezo wa kubashiri ya 10 bet, imezindua shughuli zake Afrika ikiwa ni pamoja na Tanzania.

Hatua ya 10bet kuzindua shughuli zake Afrika imekuja ikiwa na lengo la kuendeleza mpira wa miguu na mpaka sasa timu za nchi sita zitaanza kufaidika na udhamini wa kupitia kampuni hiyo.

Miongoni mwa timu hizo ni Dodoma Jiji FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, nyingine zikiwa ni Talanta ya Kenya, Enyimba (Nigeria), Aduana Stars (Ghana), Red Arrows (Zambia) na DC Motema Pembe ya DR Congo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya 10bet Africa, Arthur Perry, alisema wameamua kuingiza shughuli zao katika Bara la Afrika ili kuleta maendeleo ya kweli ya mpira wa miguu na timu hizo sita zitaingia makubaliano ya miaka mitatu kila moja. Perry alisema kampuni yao inajisikia fahari sana kuingia udhamini na timu za Afrika kwa kuwa lengo lao ni kuleta maendeleo.

"Tumehamasika sana kuingia katika makubaliano na ushirikiano wa klabu hizi, lengo ni kuleta maendeleo ya kweli katika mpira wa miguu Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Ni hatua kubwa katika kuelekea lengo ambalo tumejiwekea ikiwa ni kuwapa furaha mashabiki wa mpira wa miguu duniani kote," alisema Perry.

Alisema wameshaanza kusaidia kuendeleza vipaji katika nchi mbalimbali wakiwa na lengo kuu la kuibua wachezaji mastaa kama Mbwana Samatta na Samuel Chukwueze wa Nigeria.

Alifafanua kuwa wachezaji wengi chipukizi wanashindwa kufikia malengo yao kutokana na ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kampuni yao pia imeanza zoezi la kusaidia eneo hilo na pia kusaidia mafunzo ya makocha.

Perry amesema kuwa sambamba na udhamini, kampuni yao pia imedhamiria kuleta furaha kwa mashabiki kupitia michezo yake ya kubashiri.

"Huu ni mwanzo tu, tumedhamiria kufanya mambo mengi ya kimaendeleo katika mpira wa miguu kupitia michezo yetu ya kubashiri," alisema.

# Michezo

Jumatatu Septemba 20, 2021

Nipashe





Mane afikisha mabao 100 Liver UKURASA 22





Umati wa mashabiki wa Simba waliojitokeza katika Tamasha la Simba Day Uwanja wa Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Day babkubwa, Yanga aibu tena CAF

## ●●● Rekodi mpya yaandikwa kwa Mkapa, watani wao wapigwa na kitu kizito kichwani Nigeria huku...

**Na Adam Fungamwango**

TAMASHA la kila mwaka la klabu ya Simba, Simba Day, licha ya kufana kutokana na namna lilivyoandaliwa, lakini lilimalizika kwa Simba kuchapwa bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo, huku klabu hiyo ikiwaonyesha hadharani wachezaji wake 32 watakaowatumia kwa msimu wa ujao wa 2021/22.

**Wanachama na mashabiki wa Simba walimiminika kwa wingi na kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa, mapema tu saa 7:00 mchana hiyo ikiwa ni rekodi mpya tangu uwanja huo ujengwe, huku tiketi zote zikiwa zimemalizika.**

Wasanii mbalimbali 'walichizisha' mashabiki wake, waume, wanawake vijana kwa wazee na watoto ambao muda wote walionekana kufurahi wakipunga bendara za klabu hiyo.

Wachezaji waliotambulishwa kwenye kilele cha tamasha hilo ni Ally Salim, Gadiel Michael, Benard Morrison, Jonas Mkude, Thadeo Lwanga, Israel Mwenda, Paschal Wawa, Chris Mugalu, Rally Bwalya, Ibrahim Ajibu, Peter Banda, Shomari Kapombe, Sadio Kanoute, Meddie Kagere, Joash Onyango, Pape Sakho na Erasto Nyoni.

Wengine ni Mzamiru Yassin, Jimson Mwanuke, John Bocco, Hassan Dilunga, Abdulswamad Kassim, Aishi Manula, Kennedy, Juma, Benno Kakolanya, Duncan Nyoni, Yusuph Mhilu, Enock Inonga, Ahmed Teru, Jeremiah Kisubi na Kibu Denis.

Katika mechi ya jana, ambayo Simba ilicheza kwa mara ya kwanza bila wachezaji wake tegemeo, Luis Miquissone aliyepigwa bei Al Ahly ya Misri na Clatous Chama aliyeuzwa, RS Berkane ya Morocco, ilifika golini mwa wapinzani wao dakika ya tisa, alipotaka kumlamba chenga kipa Moukoro Ibrahim, lakini alijichanganya na mpira ukatoka nje.

Aliyetia doa sherehe za Simba alikuwa ni Beleke Jean dakika ya 83 aliyefunga bao kwa tik-tak. Bao hilo lilitokana na Manula kutoka golini kumfuata Mwape Tandi, lakini mpira huo ulipigwa langoni, kukiwa na mabeki tu, mfungaji akaukwamisha wavuni.

Sekunde chache baadaye, TP Mazembe ilijibu shambulio, baada ya Christian Kwame kuupata mpira uliokuwa unazagaa mita zipatazo 30, kabla ya kuachia shuti kali lililotemwa na kipa Aishi Manula na kukosa muunganishani.

Bwalya, almanusura aipatie Simba bao dakika ya 21, baada ya kupiga shuti kali akiwa mita takriban 25, lakini Moukoro aliuweka mpira mikononi.

Mugalu itabidi ajilaumu, alipomegewa krosi safi kutoka kwa Kapombe, lakini kwa mshangao wa wengi, akapiga mpira juu la lango.

Baada ya Simba kufungwa bao dakika ya 83, dakika saba zilizobaki Simba ilipoteza nafasi mbili za wazi ambazo ingeweza kujipatia mabao.

Dakika ya 85, Sakho alikuwa analitazama lango alipaisha mpira juu, huku dakika moja kabla mechi kumalizika, Kagere alishindwa kuunganisha krosi ya Nyoni na mpira kuwahiwa na kipa.

Awali katika mechi za ufunguzi timu ya Vijana ya Simba chini ya miaka 20 iliichapa JKU ya Zanzibar bao 1-0, huku Simba Queens ikitoka suluhu na Fountain Gates ya Dodoma.

### YANGA AIBU CAF

Safari ya wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga iliishia nchini Nigeria jana, ilipokubali kupigwa kwa mara nyingine na 'kitu kizito' kichwani kama ilivyokuwa mchezo wa awali Dar es Salaam ilipolambwa bao 1-0 dhidi ya Rivers United, kwenye mechi ya mkondo wa pili ya michuano hiyo hatua ya awali.

Kwa matokeo hayo, Yanga imetolewa kwenye hatua hiyo kwa jumla ya mabao 2-0, baada ya kufungwa bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, wiki moja iliyopita.

Kwenye mechi hiyo iliyokuwa na vigisu, Yanga kupitia msemaji wao, Haji Manara ililalamikia hujuma mbalimbali zilizofanywa na wapinzani wao akieleza wachezaji wao wanne walidaiwa kuwa na ugonjwa wa COVID-19, ambao ni Feisal Salum, Yacouba Songne, Djigui Diara, na Mukoko Tonombe. Hata hivyo, baadaye wachezaji hao walikubaliwa na kucheza.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >